# *MWANA-KONDOO NA HUA*

Bwana mwenye rehema, tunashukuru kuja mbele Zako tena, usiku wa leo, tukiwa na shukrani mioyoni mwetu, kwa yale tunayojua ya kwamba Wewe umefanya, na kwa imani kuamini ya kwamba utaendelea kutufanyia mambo mengi sana, kwa wingi. Ninakushukuru kwa yale yaliyotia nanga moyoni mwangu katika chumba hicho cha dharura sasa hivi, juu ya maskini watu hao wagonjwa, na watu wanaokufa. Ninaamini Wewe ulikomesha mauti dakika chache tu zilizopita, Bwana. Nina furaha kwa ajili ya hilo.

2 Mungu, ninaomba ya kwamba utakomesha mauti na magonjwa juu ya jengo hili usiku wa leo, kila mahali, jalia kusiwe na mtu mnyonge miongoni mwetu mwishoni mwa ibada. Tupe ushindi, Baba. Wabariki watu Wako, kila mahali. Wabariki wahudumu, wachungaji wako wa kundi. Tunaomba ya kwamba utaifariji mioyo yao sana, wasonge mbele, Bwana, wakihubiri dhihirisho kamili la Roho. Tujalie, Bwana. Bariki kila kanisa na kila mtu, jipatie Mwenyewe utukufu.

3 Hapa kuna vifurushi vingi vidogo, vimewekwa hapa, Baba, ni leso na vipande vidogo vya nguo, ambavyo wameviweka hapa vipate kuombewa. Tunafundishwa katika Biblia, ya kwamba—ya kwamba walichukua kutoka kwenye mwili wa Mtakatifu Paulo leso na nguo, na pepo wachafu wakawatoka watu, nao wakaponywa magonjwa.

4 Wala sisi si Mtakatifu Paulo, bali Wewe ungali ni Yesu, na—nami naomba, Baba, ya kwamba kama vile watu walivyokuwa na imani ya kufanya jambo hili, tupe imani ya kuamini ya kwamba maombi yao yatajibiwa. Jalia kila ugonjwa ambao leso hizi zinawakilisha, jalia umtoroke huyo mtu mara tu atakapowekelewa hizi leso. Waokoe waliopotea usiku wa leo, Baba, waponye wagonjwa, jipatie Mwenyewe utukufu, kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

5 Mnaweza kuketi. Tuna furaha sana, kwa kweli, kurudi humu jengoni usiku wa leo pamoja na ndugu zetu, na pamoja nanyi watu hapa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Nikitumaini, usiku wa leo, ya kwamba tutapata ushindi mkuu usiku wa leo, naona ya kwamba tutapata, kwa namna fulani. Nami. . .Tulikuwa na wakati mzuri sana jana jioni. Nguvu za Roho Mtakatifu, loo, mimi, sote tuliufurahia tu. . .ilikuwa vigumu kupata usingizi baada ya mimi kufika nyumbani, kuwazia tu juu ya Uwepo wa Bwana ukimpiga tu adui, ukileta ushindi. Na kuona watu wakienda kuutafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu, na mambo makuu yakitukia, utukufu wa Mungu juu ya watu, hilo linanitia moyo.

6 Mwajua, nilikuwa mchungaji wa Kanisa la Baptisti ya Kwanza huko Milltown, Indiana. Nilikaa na watu fulani huko nje mashambani wakati ningekuwa huko chini kwa ninii yangu, ilikuwa kama mzunguko, nami ningefanya uamsho, nilizoea kukaa na watu fulani walioitwa Wright.

7 Nami sikuzote nilishangaa, sijui kama mnao hapa ama la, kinega ama ndege mwigo, na nchi yetu imejaa hao. Niliwazia walinifuata kote Marekani, kila niendako, wanafuata. Ninatoka kwenda kukata nyasi zangu uani, mbona, nafungulia redio yangu, hiyo ni wale vinega, na ndege mwigo, na ndege wote wakiimba, Na—nafikiri hiyo ni redio ya Mungu, bora sana niliyopata kusikia maishani mwangu, ni kuwasikia ndege.

8 Na wavulana wengi zaidi huwatupia ndege mawe, lakini ninawazia hawa wawili walioketi hapa kwenye kiti cha mbele hawangewatupia ndege mawe. Ninaweza tu...La, bwana. Na hakikisheni hamuwatupii maskini robini wangu mawe, mnaona, naam, robini ni ndege wangu. Mliwahi kumwona na kifua chekundu? Mnajua jinsi hicho kilivyokuwa chekundu? Nitawaambia, ili kwamba hamtamtupia mawe.

9 Siku moja, kulikuwa na Mtu aliyekuwa akifa msalabani, kila mtu alikuwa amemwacha, mikono Yake ilikuwa imetundikwa msalabani, machozi ya chumvi na Damu ikitiririka kutoka usoni Mwake, akitemewa mate mwilini, Naye akapigiliwa misumari pale. Basi maskini ndege mmoja, ndege mdogo wa hudhurungi akamhurumia sana, aliendelea kuirukia mikono Yake na kujaribu kuing'oa hiyo misumari, akiirukia miguu Yake na kujaribu kuing'oa hiyo misumari. Mnajua kilichotukia? Maskini kifua chake kikawa chekundu kwa Damu, na tangu wakati huo amekuwa na kifua chekundu. Hutaki kumtupia mawe, sivyo? La, la.

10 Nami natumaini tu kwamba nitakapoenda kumlaki, pia, kwamba kifuniko changu kitakuwa na Damu kifuani pia, nikijaribu kuing'oa hiyo misumari. Nafikiri sote tunajisikia hivyo, sivyo? Dhambi zangu ndizo zilizomweka pale, laiti ningalikuwa na njia fulani ningeweza kuiondoa, bali ilibidi Yeye afe kwa ajili yangu.

11 Maskini hawa vinega walikuwa wakiketi huko chini, na kuimba usiku, na, wakati nikiingia. Nilimchunguza kinega, ninapenda kusoma maumbile, kama mjuavyo napenda maumbile, nami nilikuwa nikisoma juu ya kinega. Wakati mwingine kwenye usiku wenye dhoruba kwelikweli ataketi huko nje na ataendelea tu kuangalia juu, na mara anapoweza kuona mawingu meusi yakipita, kama anaweza kutazama aone nyota moja ndogo ataanza kuimba, kwa sababu anajua jua linawaka mahali fulani, linaakisi jua, nyota, mwezi, na kadhalika.

12 Kwa hiyo maadamu ninaweza kuona mkutano mzuri kama wa jana usiku, ninaweza tu kuendelea kuimba, maana ninajua Mwana anaangaza mahali fulani, kuliona likiakisi tena duniani, utukufu wa Mungu.

13 Sasa, ninyi mlio na Biblia zenu na mngetaka kusoma pamoja nami, hebu na tufungue Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza.

14 Na sasa, kesho usiku, natumaini ya kwamba kila Mkristo atamleta rafiki mwenye dhambi pamoja nao kesho usiku. Bwana akipenda, ninatumaini ya kwamba kesho usiku utakuwa ndio ule usiku ambao Roho atanijalia mambo ambayo nimekuwa nikiombea kwa bidii sana tangu nimekuwa mkutanoni.

15 Halafu basi, Jumapili alasiri, tuna—tunafunga uamsho huu, nami nitasema kwamba umekuwa ni wakati mzuri sana kwangu, wakati mzuri sana, bila shaka nilifurahia kukaa huku, ambapo nimengojea muda mrefu sana kuja Yakima. Na kama huna kanisa la kuhudhuria, kanisa lako halina ibada Jumapili alasiri, uhakikishe unahudhuria pamoja nasi, nasi tungefurahia ukiomba pamoja nasi, na kutusaidia safarini. Uwepo Wako unamaanisha mengi sana kwetu, na—na halafu utakuwa hapa kuomba, na kutusaidia na wengine.

16 Kila usiku, tunajaribu kuwaombea wagonjwa. Kama si wengi sana ninaweza kusimama mstarini, pia, hasa sana kwenye hayo maono nami nina hakika waaminio wanaelewa. Hii ni karibu tu awamu ya mwisho, kama ningerudi Yakima tena wakati mwingine, sitakuwa nikiwaombea wagonjwa namna hiyo, itakuwa ni zaidi ya hivyo. Mnaona? Ni karibu tu awamu yake ya mwisho, ninaweza kuihisi inapoanza kutoka, imekuwa ni kuuzunguka ulimwengu kabisa, mara tatu ama nne sasa. Kwa hiyo ni ninii. . . haitachukua muda mrefu mpaka huduma hiyo itakapoondoka, na itakuwa ni mpya ambayo itakuwa mbali sana kupita hii.

17 Na wakati nikiwa hapa mara ya kwanza, Hiyo iliwaambia *hii* inakuja, (Ni wangapi walio humu jengoni, walionisikia nikitangaza hilo huko nyuma katika siku za mwanzoni? Inueni mikono yenu, popote mlipo. Hakika. Mnaona?), huko nyuma kabisa kwamba hii ingekuja, hivi si ilikuja? Jinsi hasa Yeye alivyosema ingekuja. Sasa, kuna nyingine inayokuja ambayo itakuwa mbali zaidi kupita hii, nayo itakuwa ni kubwa, nina hakika. Laiti ningalijua ilikuwa ni nini, bali sijui, ninajua tu inakuja.

18 Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza, na hebu tuanzie kwenye kifungu cha 29 tusome sehemu yake tu, kutoa somo kwake:

> *Siku ya pili yake Yohana amwona Yesu anakuja kwake,* akasema*, Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.*

*Huyu ndiye. . .niliyenena habari zake ya kwamba, Yuaja mtu nyuma yangu, ambaye amekuwa mbele yangu, kwa maana alikuwako kabla yangu.*

*Wala mimi sikumjua: lakini kusudi adhihirishwe kwa Israeli, ndiyo maana mimi nilikuja nikibatiza kwa maji.*

*Tena Yohana akashuhudia, akisema, Nimemwona Roho akishuka kama hua kutoka mbinguni, naye akakaa juu yake.*

19 Kwenye mifano hii, usiku wa leo, ningetaka kuchukua somo la *Mwana-Kondoo Na Hua*.

20 Mnajua, kondoo ni mwepesi sana kuathirika na wa kipekee. Na, mwajua, kondoo kamwe hakuombwa kutengeneza sufu, aliombwa kutoa sufu, kwa sababu yeye ni kondoo. Na maadamu yeye ni kondoo atatoa sufu, kwa sababu hiyo ndiyo asili yake. Basi ndivyo ilivyo kwa Kanisa la Kikristo, kamwe hatukuombwa tutengeneze matunda, tuliombwa kuzaa matunda.

21 Wagalatia 5 ilisema, "Tunda la Roho ni upendo, furaha, imani, amani, uvumilivu, upole, upole, subira." Hizi hazipaswi kutengenezwa, zinapaswa kuwa bidhaa zinazotoka ndani kwenda nje. Maisha ya nje tunayoishi, yanathibitisha kilicho ndani.

22 Sasa, tumejaribu kutengeneza hili, kutengeneza matunda ya Roho, na daima tunageuka kuwa unafiki, kwa sababu huwezi kutengeneza Ukristo, ni tukio la Roho anayeishi ndani yako, na kuzaa tunda lake Lenyewe, huwezi kulitengeneza. Tumejaribu kulielimisha, na kuliundia dhehebu, na tunapofanya hivyo tunageuka kuwa unafiki na kushindwa. Halipaswi kufanywa hivyo, linapaswa kufanywa jinsi Mungu alivyokusudia li—lifanywe, Roho aliye ndani yetu akizaa matunda ya Uwepo Wake. Huo ndio mpango wa Mungu, hauwezi kubadilishwa kamwe.

23 Na hili, usiku wa leo, ni somo lisilo la kawaida sana, lakini Mungu si wa kawaida, Naye hufanya mambo kwa njia isiyo ya kawaida, katika wakati usio wa kawaida, pamoja na watu wasio wa kawaida, Yeye kwa jumla si wa kawaida. Nami nafikiri huu ni mmojawapo wa mifano ya kuvutia sana ya Maandiko yote, wakati lilipompendeza sana Mungu, hata alipotaka kumwashiria Mwanawe duniani, aliitwa Mwana-Kondoo, "Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Ndipo basi wakati Yeye, Mungu, alipokuwa akitaka kujifananisha Mwenyewe aliwakilishwa na Hua.

24 Sasa, kama utaangalia, kati ya viumbe vyote vinavyozurura duniani hakuna kitu kilicho kipole na kinyenyekevu kama mwana-kondoo, hakuna kitu kisicho na hatia kama mwana-kondoo, kipole, kinyenyekevu. Na kuhusu hua, hakuna ndege anayeruka kwenye anga za mbinguni, mpole na mnyenyekevu kama hua. Ndiye ndege mwepesi wa hisia sana kuliko ndege

wote; naye mwana-kondoo ndiye mwepesi wa hisia sana kuliko wanyama wote.

25 Kwa hiyo, kama utaangalia, mwana-kondoo na hua wana roho sawa na asili sawa. Kama isingalikuwa hivyo, kama kunguru angalimrukia huyo mwana-kondoo, mwana-kondoo asingeweza kustahimili hilo. Na kama hu—hua angeruka chini aje juu ya mbwa mwitu, huyo hua hangalistahimili hilo, asili zao hazikuwa sawa. Kwa hiyo ilibidi iwe ni mwana-kondoo na mbwa mwitu, ama, mwana-kondoo na hua wakifananishwa pamoja, Mungu na Mwanawe, ili kwamba waweze kuishi pamoja.

26 Sasa, mara nyingi nimeshangaa ni kwa nini Mungu aliwahi kutuwakilisha kama wana-kondoo, sisi ni kondoo wa malisho Yake. Kama ukiangalia, mwana-kondoo ni mmoja wa wanyama wasio wa kawaida sana, mwana-kondoo huyo hawezi kupata njia ya kurudi wakati amepotea. Nimefuga kondoo, na hebu kondoo apotee, atasimama hapo na kulia mpaka afe, hawezi kupata njia ya kurudi, hana budi kuwa na mchungaji wa kumrudisha.

27 Na kamwe hatutapata njia ya kurudi kupitia njia nyingine yoyote ila kupitia kwa yule Mchungaji. Jamii ya binadamu imepotea, inahitaji kuchungwa irudishwe. Hatuwezi kupata njia yetu ya kurudi kupitia mipango ya elimu, hatuwezi kupata njia yetu ya kurudi kupitia sayansi, hatuwezi kupata njia yetu ya kurudi kupitia dini, kuna njia moja tu ya kurudi, na hiyo ni kwa Mchungaji.

28 Hua, yeye ni ndege asiye wa kawaida kabisa, hua ndiye ndege pekee tunayemjua ambaye hana nyongo. Hua hana nyongo hata kidogo, ndege wengine wote wana nyongo, bali yeye hana nyongo, kwa hiyo ndani ya hua hamna uchungu. Pia ndani ya Mungu hamna uchungu, ama katika yule Hua anaishi ndani yake na kumwongoza, hamna uchungu. Sasa, hua, sababu ya yeye kuumbwa namna hiyo, ni kwa sababu ya mlo wake. Sasa, asingeweza kula vitu vinavyoliwa na koho, kwa sababu vingemwua mara moja.

29 Na jambo lingine ningetaka kuzungumza kuhusu hua, papa hapa, ni kwamba hua ni mmoja wa ndege walio safi sana walioko wanaoruka angani. Hakuna kitu kilicho safi kama hua, wala haimbidi kuwa mwangalifu kuuhusu, mwili wake unatoa mafuta yanayoingia kwenye manyoya yake na daima yanamdumisha safi.

30 Loo, ni mfano wa jinsi gani, ya kwamba mwaminio ana Mafuta ya Roho aishiye ndani yake, anadumisha manyoya yake safi! Mavumbi na kadhalika hayamsumbui hua, maskini mwili wake umejaa mafuta, nayo humkinga na mavumbi na kadhalika, yanatiririka sikuzote. Naye anaporuka mavumbi yanamwondokea, hayawezi kunatia juu yake, kwa sababu

mafuta fulani haya hutoka kwake kwa kusudi hilo, wala uchafu hauwezi kunatia juu yake. Ni mfano wa jinsi gani!

31 Ee Mungu ijaze taa yangu usiku wa leo, kwa Mafuta ya namna hiyo, hata ulimwengu na anasa zake zote, na utajiri wake, na madoido yake makuu havitatunatia sisi, hata tutaweza kuvitupilia mbali kwa Mafuta yanayotoka ndani, yakifanya kazi kulidumisha Kanisa safi.

32 Kama vile ule wimbo wa kale ulivyokuwa ukisema, "Nipe Mafuta katika taa yangu, niendelee kuangaza." Mungu huweka Mafuta Matakatifu ndani. Mafuta katika Biblia yanawakilisha Roho akilidumisha Kanisa safi.

33 Na hata hivyo, hua ni ndege, yeye ni, ndege tu, naye hua amewakilishwa katika Biblia kote tangu Mwanzo hadi Ufunuo. Nimemchunguza sana huyo ndege. Katika nchi yetu na karibu majimbo yote katika huu Mwungano yeye ni ndege mtakatifu. Haturuhusiwi kumwinda, lakini katika baadhi ya majimbo wanaruhusiwa kumwinda; nisingeweza kupiga risasi hata mmoja. Lakini yeye ni ndege mtakatifu katika jimbo letu, wangekutoza faini ya dola mia moja mara tu ukimwua mmoja, yeye ni ndege mtakatifu.

34 Sasa, ndani ya safina hua na kunguru waliketi kwenye kijiti kile kile, wote wawili walikuwa ndege, mmoja angeweza kuruka mahali ambapo huyo mwingine aliruka, mmoja angeweza kufanya lolote tu huyo mwingine angeweza kufanya, lakini walipoachiliwa wakajichagulie, walimwachilia hua kwanza, ndipo maskini jamaa huyo akaruka kote, nayo Biblia ilisema, "Hakuona mahali pa kutua kwa nyayo za miguu yake." Kila wakati alipoweza kupata kitu cha kutulia, kilikuwa ni mzoga uliokufa, maskini kitu fulani kilichokufa cha ulimwengu, naye asingeweza kukikalia hicho. Mbona, kilikuwa kinyume na maumbile yake.

35 Na kama mtu akipata kuzaliwa na Roho hiyo ya Hua ndani yake, sisemi hataondoka, jambo fulani huenda likatukia angeruka mahali fulani, lakini kama kweli alikuwa na hiyo Roho ya Hua, hatapata raha kwa nafsi iliyo ndani yake. Ewe mtu uliyerudi nyuma, wewe ndiwe mwenye mashaka sana ulimwenguni, huwezi kupata raha, mahali popote. Utasikika kama, ushuhuda wako kama Petro alivyosema, "Twende kwa nani? Twende wapi? Wewe Ndiwe pekee uliye na Maneno ya Uzima wa Milele."

36 Naye Mkristo halisi, aliyezaliwa mara ya pili wakati mwingine huenda akakasirikia jambo fulani linalofanywa kanisani, itatia sumu mfumo wake, lakini kama yeye ni hua halisi, atarudi, hakika tu kadiri Mungu alivyo Mbinguni, atarudi, kwa sababu kuna kitu ndani yake ambacho hakitamwacha ashuke kwenye mizoga hiyo iliyokufa, aende kwenye karamu ya roki, ama kilabu cha pombe, hayo kwake

yananuka tu, kwa Mkristo yeyote aliyezaliwa mara ya pili, kamwe hawawezi kuvumilia hilo, kwa sababu hana nyongo ndani yake ya kumeng'enya kitu kama hicho.

37 Naam, lakini walipomwachilia huyo kunguru, loo, alishangilia tu alivyoweza, akiruka kutoka kwenye mzoga mmoja uliokufa hadi mwingine na kula na kulijaza tumbo lake kabisa; hivyo ndivyo kunguru wafanyavyo. Naye kunguru ni mnafiki. Nina furaha mna msimu wazi juu yake kila mahali. Naye ni jamaa mbaya sana, anayeishi muda mrefu, ila anaweza kuketi juu ya mzoga wa kale uliokufa, na kula kiasi atakacho, na kuruka moja kwa moja kondeni na kula ngano pamoja na hua. Lakini hua akila ngano hawezi kuruka arudi na kula pamoja naye.

38 Kwa hiyo, mnafiki anaweza kwenda kanisani, na kupaza sauti, na kupiga makelele, na kuandika jina lao kwenye kitabu, atoke nje na kufurahia michezo ya karata, kunywa pombe, kuvuta sigara, kucheza dansi, roki, na mambo hayo yote, na kurudi kanisani na kula Chakula kutoka kanisani.

39 Nilishangaa kuhusu hilo wakati mmoja, nikaona ono, ilidhihirishwa jinsi ambavyo ninii...Mtu mmoja alitoka akaenda kupanda ngano, wakati alipolala, mbona, basi adui akatokea, akapanda magugu, ambalo ni la Kimaandiko. Basi ngano ilipochipuka, na ninii, ilipoiva, kwekwe zilikuwa zimeota pia, magugu.

40 Basi wakati ukame ulipokuja, na wakati ukame ulipokuja kila mtu alikuwa akiomba kwa ajili ya mvua, ndipo wingu kubwa jeusi likaja na kunyesha. Na maskini ngano hiyo ilikuwa imeinamisha kichwa chake namna *hii*, ikainua maskini kichwa chake juu na kuanza kusema, "Loo, utukufu kwa Mungu! Bwana asifiwe kwa kuleta mvua!"

Ndipo lile gugu dogo likaruka juu kama tu vile ngano ilivyoruka, na kusema, "Utukufu kwa Mungu, haleluya, kwa kuleta mvua!"

41 Nikasema, "Sasa, sijui la kuwazia." Ndipo nikaona basi tena ya kwamba mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki. Mvua ilitumwa kwa ajili ya ngano, lakini magugu yakiwa mle ndani yalifaidika nayo, mvua ile ile, lakini, "Kwa matunda yao mtawatambua," alisema Yesu.

42 Sio jinsi tunavyojiunga na kanisa, na jinsi tulivyo waaminifu kwa *hili*, *lile*, ama *linginelo*, tunda la Roho ndilo muhimu, ndilo linalomwonyesha mwanamume au mwanamke kile walicho, Kitu fulani ndani yao, si kujibunia, bali wanakizaa, ule Uhai uliokuwa ndani ya Kristo uko ndani yako, unajionyesha Wenyewe. Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao walio, wanaoamini." Kitu kisicho cha kujibunia, kilichoelimishwa kwa theolojia, bali ni Roho ya Roho Mtakatifu katika moyo

wa mwanadamu, kikizaa matunda na ushuhuda wa kufufuka Kwake na nguvu Zake zilizo hai.

43 Loo naam, hua ni ndege wa kupendeza. Nimekuwa na uhusiano mwingi nao. Wakati mmoja, nilipoenda kumwombea Florence Nightingale, nyanya wa nyanya yake alianzisha Shirika la Msalaba Mwekundu, nanyi mna picha yake hapa katika kitabu kiitwacho *Nabii Azuru Afrika*, kilichoandikwa na Julius Stadsklev.

44 Basi nilipoingia London, ndege ilitua nami nikawasikia wakiniita katika . . . Walikuwa na wasindikizaji wote huko nje, ndipo mtu fulani akasema, "Kuna mama anayekufa hapa, katika ndege, ndiyo kwanza aletwe kutoka Afrika Kusini."

45 Vema, ni—nisingeweza kwenda kule, nisingeweza kuupenya huo umati. Nami nikamtuma mtu aende pale, akaseme tungempeleka mahali pengine mara tu baada ya kwenda na kufanya wajibu wangu wa kwenda kule, kuomba, kumwombea mfalme, na kadhalika. Nikarudi kwenye Hoteli ya Piccadilly, ndipo wangeweza kukutana nami kule.

46 Basi nilipoingia chumbani, kwa mwanamke huyu, alikuwa ameniandikia barua, Binti Florence Nightingale, naye alitaka nije nimwombee, nisingeweza kufanya hivyo. Alikuwa tu na uzito wa ratili sitini.

47 Na kama mtaiangalia hiyo picha, ilitubidi kuifunika na kitu fulani *hivi* tupate kupiga picha, Ndugu Lindsay akafanya hivyo, kwa sababu ilikuwa ni kipande kidogo cha kumfunika. Viungo vyake vilikuwa vikubwa *hivi* tu kote, juu karibu na nyonga, mishipa ilikuwa imebonyea. Jinsi huyo mwanamke alivyokuwa akiishi, sijui.

48 Nikaingia chumbani, naye alikuwa katika parokia moja nyuma ya kanisa, naye alikuwa na wauguzi wawili, nami nikasema, "Je, wewe ni Binti Nightingale?" Ndipo nikaangalia na taya zake zilikuwa zimezama ndani, mifupa yake ya mashavu imetokeza, na hiyo ilikuwa kama sehemu ya mraba ya fuvu la kichwa, mahali kinaposhikamanishwa palikuwa wazi, hakuna nyama hata kidogo.

49 Ndipo akaanza kulia, nikashangaa ni wapi hata kungeweza kuwa na unyevu wa kutosha hata aweze kulia. Akala glukosi, nayo matumbo yake yote yalikuwa na kansa tumboni mwake. Jinsi huyo mwanamke alivyokuwa akiishi, sijui. Nisingeweza kuelewa hata kidogo, alikuwa akisogeza midomo yake, ndipo nesi akashuka kuona kile alichosema, ndipo akasema, "Mwambie Ndugu Branham amwombe Mungu anijalie nife."

50 Loo, nikajaribu kumshika mkono, ndipo nesi akauinua mkono wake, na kuweka umbo hilo la mifupa iliyokufa na mishipa yake mikononi mwangu, baridi iwezavyo kuwa, na vifundo na viungo vimeshikana *tu* pamoja. Ni hisia ya jinsi gani ya mwanadamu aliyelala namna hiyo!

51 Nisingeweza kumwombea afe huku nikiwa huko nikiwaombea wagonjwa wapate afya. Kwa hiyo nikawaomba wahudumu, kulikuwa na saba ama wanane chumbani, nami nikasema, "Hebu tupige magoti."

52 Na huko Uingereza, kama mtu yeyote amewahi kuwa kule, wakati ukungu unapoingia, kamwe huwezi kuona chochote, hiyo ilikuwa ni siku yenye ukungu sana, ilibidi teksi iendeshwe kwa uangalifu sana iwezekanavyo kupitia kwenye huo ukungu. Na kulikuwako na wimbi kubwa lake lililoingia, tulikuwa karibu na pwani, na kulikuwa na ukungu sana ningeweza *tu* kuona kulikuwa na mti uliosimama karibu na dirisha.

53 Nilipopiga magoti kando ya dirisha, kizingiti kilikuwa karibu umbali *huo* juu, hata kwa uso wangu, nami nikaanza kuomba. Na nilipoanza kuomba, "Mwenyezi Mungu, Mwanzilishi wa Uzima wa milele, Mpaji wa vipawa vyote vizuri. Tuma juu ya maskini kiumbe hiki kinachokufa, hapa, baraka Zako."

54 Nilipoanza tu kuomba, maskini hua mdogo akaruka akaingia kutoka mahali fulani, akatua kwenye kizingiti hiki, akaanza kutembea huku na huko, akipiga kelele, yapata futi moja tu kutoka mahali uso wangu ulipokuwa, nikiomba. Nami nilifikiri alikuwa ni ndege wa kufuga pale nyumbani, nilikuwa ndiyo kwanza niingie Uingereza yapata saa nne ama tano, nami nikawazia, labda, alikuwa tu ni aliyefugwa pale nyumbani. Naye akatembea huku na huko, huku na huko kwenye maskini kizingiti hiki. Ndipo basi hatimaye nilipoomba na kusema, "Amina," na kusimama, maskini yule hua akaruka akaenda zake.

Nami nilikuwa nikitaka kusema, "Je, huyo alikuwa ni hua wa kufuga?"

Nao hao wahudumu walikuwa wakizungumza juu ya, "Huyo hua alikuwa akifanya nini pale?"

Vema, nikasema, "Je, ni hua wa kufuga?"

Nao wakasema, "La." Hawakuwa wamewahi kumwona hapo kabla.

55 Ndipo nikageuka kumwangalia huyo mwanamke, pale mbele yangu alisimama mwanamke mwenye nguvu, mwenye afya, nikasema, "BWANA ASEMA HIVI: Utaishi wala hutakufa."

56 Hebu fungueni ukurasa unaofuata kwenye hicho kitabu na mumwangalie mwaka mmoja baadaye, yeye anafanya uuguzi sasa huko Uingereza, mwenye nguvu, mwenye afya. Mungu katika mfano wa hua alitua dirishani, akamtuma mjumbe Wake.

57 Mnajua hadithi yangu, msichana wangu mdogo, mke wangu wakati walipokufa. Kila jioni ningeenda huko nje kwa muda mrefu kaburini, na kuketi huko juu, na, loo, kamwe nisingeweza kuwaachilia, ilikuwa vigumu, nilikuwa mvulana tu, na familia

yangu yote imekwisha, mimi na Billy tu ndio tuliosalia. Nami sikuninii . . . Ningeenda huko nje na kuketi kaburini, na kila alasiri, hakika tu kama ilipokaribia yapata saa kumi na moja, huyu hapa maskini njiwa anakuja, akiruka kichakani, akatua kwenye mmojawapo wa hiyo mierezi huko nje, na kupiga tu kelele na kuimba. Ningeinua mikono yangu, na kumsifu Bwana, ilisikika kama upepo ukishuka kupitia kwenye hivyo vichaka, na kuimba:

> Kuna Nchi ng'ambo ya mto,
> Wanayoiita tamu milele,
> Nasi tunafika tu kwenye Pwani hiyo kwa agizo la imani;
> Mmoja mmoja tunafika malangoni,
> Huko tukaishi pamoja na wasiopatikana na mauti.
> Siku moja watapiga hizo kengele za dhahabu kwa ajili yangu na yako.

58 Maskini yule hua akipiga kelele, kwanza nilifikiri ilikuwa ni nafsi isiyopatikana na mauti ya—ya msichana wangu mdogo, lakini kama ingalikuwa ni yeye angekuja azungumze nami. Lakini huyo hua, Mungu alijiwakilisha Mwenyewe katika kufanyika hua.

59 Sasa mwana-kondoo, sasa, hua hutoa mafuta apate kujiweka safi, naye mwana-kondoo ana lanolini kujikinga na hali ya hewa. Nasi tunafananishwa na wana-kondoo wa Mungu.

60 Ninawatakeni mwone huyu alikuwa ni Mwana-kondoo wa aina gani. Mwana-kondoo huyu, mwana-kondoo hana budi kuongozwa, naye Mwana-kondoo huyu wa thamani tunayewazia habari zake, Yeye aliongozwa, "Si mapenzi Yangu, Yako yatendeke," akaongozwa hadi machinjoni.

Wakati mwingine wao . . . Mtu fulani alisema, "Kwa nini Yesu aliongozwa mpaka Kalvari?"

61 Mnajua Biblia ilisema walimpeleka, wakamfunga kamba shingoni na kumpeleka. Kwa nini? Alikuwa ni Mwana-kondoo wa Mungu. Kwa nini akazaliwa katika hori? Kwa sababu Yeye alikuwa ni Mwana-kondoo, ilibidi azaliwe zizini, Yeye alikuwa ni Mwana-kondoo, alizaliwa Mwana-kondoo, na akaongozwa hadi machinjioni.

62 Uliwahi kwenda karibu na machinjio? Wanapoenda kuwachinja kondoo ni kitu gani kinachowaongoza hadi machinjioni? Mbuzi. Wana mbuzi pale ambaye atawaongoza kondoo hawa mpaka afike moja kwa moja mahali fulani, naye ataruka na kuwaacha kondoo waingie ndani. Hivyo ndivyo imekuwa daima, huyo ndiye aliyemwongoza machinjioni Mwake, mbuzi. Na ninii . . .

63 Vema, kama ukifikia wakati, wachinjaji wameniambia, wale wachinjaji waliowachinja walisema kama iliwabidi kumwua huyo mbuzi, basi alisababisha vurugu kweli. Lakini anataka kuwaongoza kondoo, sikuzote, machinjioni. Hivyo ndivyo ibilisi hulifanya, yeye daima anajaribu kuwaongoza watu wa Mungu machinjioni, kwenye baa, klabu ya usiku, mahali fulani.

64 Nawatakeni mwone, isitoshe, bali Yeye alikuwa ni Mwana-kondoo aliye tayari, Mwana-kondoo aliye tayari. Mwana-kondoo ana kitu kimoja tu, na hicho ni manyoya yake, sufu yake iliyo juu yake, bali yeye—yeye ni mwana-kondoo aliye tayari, yote aliyo nayo yuko tayari kuyaachilia. Anaachilia sufu yake, hicho ndicho kitu pekee alicho nacho, lakini hata hivyo, kwa ajili yako na kwa ajili yangu, yeye huachilia kile alicho nacho.

65 Sasa, kama tunajiita, wana-kondoo, wana-kondoo wa Mungu, tuko tayari kuachilia mawazo yetu kumfuata Mungu, tuko tayari. Lakini, loo, sisi Wamarekani hatuwezi kuongozwa, la. "Ah, bwana, tulienda shuleni, na tukajifunza jinsi ya kuongoza, hatuwezi kuongozwa. Tulijifunza Ph.D. yetu, na L. maradufu D., na kadhalika, nasi tunajua yote kulihusu, nasi tunajua jinsi ya kuongoza, kwa hiyo Hua hawezi kutuongoza."

66 Tunapokuwa na mtazamo wa namna hiyo, mbona, hatuwezi kuongozwa, inatubidi kuwaongoza watu. Lakini Mungu ana Kiongozi mmoja kutoka kwenye ninii Yake. . .kwa ajili ya Kanisa Lake, na huyo ndiye Hua, Roho Mtakatifu, ndiye Kiongozi wa watu wa Mungu, Kiongozi. Lakini tunapofikia kujua mengi sana, tunajua theolojia nyingi sana basi mwana-kondoo hawezi kutuongoza, kwa sababu ni kinyume na mawazo yetu, nasi kamwe hatutalivumilia, inakubidi kuachilia wazo lako.

67 Watu husema, "Loo, siku za miujiza zimepita, tulijifunza hayo shuleni. Mbona, tunajua hakuna—hakuna—hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu, hakuna Roho Mtakatifu kama vile Wapentekoste wanavyosema wanaye, siku hizo zimepita, nilijifunza hayo shuleni."

68 Mungu atakuongozaje basi, ukiamini kitu kama hicho? Mungu atakuponyaje, wakati unafikiri siku za miujiza zimepita? Kamwe hawezi kukuponya.

69 Kwa hiyo basi tunaendelea na kusema, "Vema, naam, tuna makanisa, na tuna mashirika makubwa, na madhehebu," bali yote yakiwa na mfano wa utauwa, bali wakimkana Hua, yule Hua aongozaye. Tuna dini zetu, na tuna mawazo yetu, wala hatutaki chochote kuchanganyikana nayo, wanasema, "Sijali Biblia inasema nini." Watu wameniambia hivyo mara nyingi.

70 Jamaa fulani, si muda mrefu uliopita, alisimama na kuniambia, kasema, "Sijali ungefanya matukio mangapi ya uponyaji, bado siuamini."

71 Nikasema, “Bila shaka, haukuwa kwa ajili ya wasioamini, ulikuwa ni kwa ajili ya waaminio.” Huyo ndiye mtu pekee ulio kwa ajili yake, ni kwa ajili yao wanaouamini, kamwe haukukusudiwa kwa ajili ya wasioamini. Naye Mungu anaweza tu kumwongoza mwanadamu, kadiri atakavyomruhusu aongoze, Mungu anaweza tu kufanya kazi na mtu yeyote atakayemruhusu Yeye kufanya kazi pamoja naye. Sikuzote nilimsikitikia Mungu akijaribu kumpata mtu ambaye angeweza kumwongoza na kufanya kazi kupitia kwake.

72 Nilikuwa, si muda mrefu uliopita, nikisoma juu ya Samsoni, na jinsi ambavyo mtu huyo, alikuwa kitu kama watu wengi wa siku hizi, mwanamume wa wanawake, wala Mungu kamwe asingeweza kumtumia. Mbona, alikuwa tayari kusalimisha nguvu zake kwa Bwana, lakini kamwe hakuwa tayari kumtolea Bwana moyo wake. Sasa, alikuwa na nguvu nyingi.

73 Na makanisa mengi siku hizi, yatamtolea Bwana nguvu zao, “Loo, hakika, tutajenga dhehebu ambalo litaingiza milioni moja ndani, na kufanya *haya* yote, *yale*, na *mengineyo*,” lakini hawako tayari kamwe kuusalimisha moyo wako kwa uongozi wa Kiungu wa Roho Mtakatifu kutuongoza kwenye chemchemi za maji ya Uzima, kamwe hatuko tayari kufanya hivyo.

74 Inaonekana kana kwamba ndilo jambo gumu kuliko yote kwa watu kuliingiza kichwani mwao kwamba Roho Mtakatifu *huongoza*. “Wana na binti za Mungu wanaoongozwa na Roho wa Mungu,” si maaskofu, na makadinali, na kadhalika, “na Roho wa Mungu,” hilo lilikuwa ndilo wazo la Mungu. Kama wewe ni mwana-kondoo, unaongozwa na Roho wa Mungu.

75 Lakini nashangaa wakati mwingine, mbele ya haya yote, kama Mungu angeweza kutuongoza. Nashangaa kama hatujakuwa mbuzi badala ya kondoo. Hua asingeweza kumwongoza mbuzi, *asingemwongoza*, la, la, anataka kuongoza, mbuzi ataongoza, bali huwezi kumwongoza. Na huenda nikakwambia jambo fulani, ndugu, hakika itakubidi kuwa mchungaji mwerevu sana kama unaweza kusikia mlio wa mbuzi na mlio wa kondoo na kuitofautisha, yote miwili inasikika karibu sawa.

76 Nayo Biblia ilisema ya kwamba ibilisi katika siku za mwisho hapa, angekuwa mjanja sana hata ingewadanganya walio wateule, kama yamkini. Jinsi Shetani atakavyoingia kwa ujanja! Angalieni tu kile kinachokaribia kutukia sasa katika siku za mwisho, angalieni chaguzi hizi na kadhalika zinazokuja, angalieni jinsi Shetani atakavyotekeleza hilo, akijaribu kuwapumbaza, alilijaribu wakati mmoja hapo awali na akashindwa. Atajaribu mpaka afanikiwe kufanya hivyo, atafanya hivyo. Naam, bwana, atafanya hivyo.

77 Basi kumbukeni, nilibashiri hilo katika mwaka wa 1933, na itakuwa hivyo, pia, kwa kuwa niliona ono kabla ya wakati wa

mwisho, kitu hicho kikuu, chenye nguvu kilisimama Marekani nayo ikawa kama makapi, kwa hiyo basi, litatukia. Nikasema, “Magari yatakuwa na umbo kama la yai.” Mnajua jinsi gari la mwaka wa ’33 lilivyoonekana. Nami nikasema, “Hata watakuwa wakisafiri barabarani, hata haitawabidi kuliongoza.”

78 Tayari wamelitoa hilo, nililiona hapa si muda mrefu uliopita, litadhibitiwa na kitu kama umeme, ama kwa nguzo ya sumaku, kupunguza mwendo wao, na kadhalika, na kuongeza mwendo wao, hayawezi kugongana, na kadhalika. Nami nimeandika hayo katika kitabu tangu 1933. Na itakuwa hivyo, tunalifikia sasa. Tuko moja kwa moja ndani yake, kwa sababu Roho Mtakatifu Ndiye anayeliongoza Kanisa, na kutuonya juu ya hatari zijazo.

79 Sasa, tunaona katika makanisa yetu, siku hizi, mambo yanayoendelea. Sasa, ilikuwa ni muda mrefu... Sasa, msinikasirikie sasa, Ninataka kuwaonyesha. Sasa, tunazungumza kuhusu huko nje katika madhehebu, sasa tutakuja nyumbani kwa Pentekoste kidogo tu. Tutashangaa ni kitu gani kimetendeka katika watu wetu wa Kipentekoste.

80 Mwajua, lilikuwa ni jambo baya sana kwa wanawake wetu kukata nywele zao, lilikuwa ni jambo baya sana. Ninaweza kukumbuka hilo, nimekuwa tu pamoja nao kwa miaka michache tu. Lakini sasa ni sawa, wanakata nywele zao. Nayo Biblia ilisema ya kwamba nywele za mwanamke zilikuwa kwa ajili ya utukufu wake. Nayo Biblia ilisema ya kwamba mwanamke akikata nywele zake, anakiaibisha kichwa chake, ambacho ni mumewe. Na kama akikata nywele zake, mumewe basi ana haki ya kumwacha mwanamke huyo asiye na heshima. Hayo ni mafundisho ya Paulo katika Wakorintho, unaweza kuyabishania naye. Sasa, najua hilo linaumiza.

81 Mama alikuwa akituchukua, naye alikuwa akiniambia, yeye...kila Jumamosi usiku ingetubidi, tungeogea kwenye beseni la kale la mwerezi. Nami nilikuwa ndiye mwenye umri mkubwa kuliko wote, na hao wanane waliogea kwenye beseni lile lile mbele yangu, nao waliongeza tu maji kidogo ya moto ndani yake. Ndipo basi kila Jumamosi usiku, jinsi ilivyotubidi kula, ilitubidi kunywa dozi ya mafuta ya mbarika; siwezi kuyavumilia, hata leo. Nami ningemjia nimeyazibia kinywani, nikishika pua yangu, ndipo nikasema, “Mama, siwezi kuvumilia kitu hiki!”

Akasema, “Kisipokuchefua kabisa, hakikufai kitu.”

82 Hiyo ndiyo njia ya kuihubiri Injili, kama haikuchefui kidogo, ikufanyie jambo fulani, haikusaidii sana. Lakini hiyo ndiyo kweli. Wanawake wetu wengi wa Kipentekoste wamefikia ambapo wanavaa maskini nguo hizi fupi kukata nyasi uani, na kadhalika, wanawake wa Kipentekoste wakiwaachilia wasichana wao wadogo, wakifanya hivyo.

83 Wanazungumza juu ya kuharibika kwa vijana, ni kuharibika kwa wazazi, shida ndiyo hiyo. Halafu kuzungumzia suala la ujinga wa Kentucky, baadhi yao hao maskini akina mama huko nje, hebu binti yao aingie vile baadhi ya wanawake wafanyavyo, saa kumi na moja alfajiri, huku wamechafua uso wao, nazo nywele zao zimechafuliwa namna *hiyo*, angechukua tawi kutoka kwenye mhikori, kisha angemtoa nguo zilizosalia na kumtoa ngozi kwa hilo, halafu ati mnaliita hilo ujinga. Mungu anajua tunahitaji mama wengine kama hao. Hiyo ni kweli kabisa.

84 Nao wanawake wetu walifikia mahali, wanavuta sigara.

Mnasema, "Vema, sasa, ngoja kidogo, mhubiri! Hiyo ni haki yangu ya Marekani."

Ninajua, lakini kama wewe ni mwana-kondoo, utaiachilia.

"Mbona, mimi ni mfuasi wa kanisa *Fulani-lile*."

Vema, kama wewe ni mwana-kondoo utaachilia haki zako.

"Mbona, ninaona hao wengine wote . . ."

Naam, hiyo ni kweli, lakini wewe ni tofauti, iwapo wewe ni Mkristo huna budi kuwa tofauti.

Mama fulani alisema, "Mimi sivai kaptura, huvaa suruali ndefu."

Nikasema, "Hizo ni mbaya zaidi." Sawa. Biblia ilisema ni chukizo kwa mwanamke kuvaa vazi limpasalo mwanamume.

85 Nilizungumza hayo katika mmojawapo wa mikutano juu ya jambo hili, ndipo mwanamke mmoja akaniandikia barua kubwa, ndefu, akasema, "Sasa, ngoja," kasema, "unapotoka kuingia kwenye fundisho la kujibunia." Kasema, "Mwanamke atafanya nini wakati akiwa huko nje amepanda farasi katika eneo lililojaa mbu, akiwakusanya ng'ombe?"

86 Nikamjibu tu, nikasema, "Hiyo si kazi ya mwanamke. Kama angeshikilia mahali pake, haingembidi kuwa huko nje." Hiyo ni kweli kabisa. Um-hum. Hiyo ni kweli kabisa. Shida yake sasa ni . . . Nawapenda dada zetu, na hiyo ni kweli, Nafikiri wako sawa, bali wanapaswa kujua mahali pao.

87 Na, mwajua, ninakumbuka wakati lilipokuwa jambo baya sana kwa wanawake wetu wa Kipentekoste kujipaka hii rangi ya makucha, mwajua, nyusoni mwao. Nimekosea hilo, daima ninakosea hilo. Ati nini . . . ? [Ndugu mmoja anasema, "Vipodozi."—Mh.] Vipodozi, vipodozi. Rangi ni za makucha. Hiyo ni kweli? Sijui chochote kuhusu upuuzi huo. Lakini kujipodoa, ilikuwa ni vibaya kwa mwanamke kujipodoa kwa rangi za kujipaka, lakini sasa wanafanya hivyo.

88 Mwajua, mzee mhudumu Mmethodisti alizoea kuimba wimbo,

> Tulilegeza kamba, tulilegeza kamba,
> Tukapatana na dhambi.

Tulilegeza kamba, kondoo wakatoka,
Lakini mbuzi waliingiaje?

89 Mlilegeza tu kamba. Mara nyingi, si ndugu hawa, bali mara nyingi, wahubiri hufikiria zaidi juu ya riziki, kuliko wanavyoifikiria Injili. Mwinjilisti anapitia. . . Inakuwa ni aibu. . .

90 Sasa, mwinjilisti mmoja aliniambia, mwinjilisti mashuhuri hivi majuzi, kasema, "Utaidhuru huduma yako."

Nikasema, "Chochote kitakachodhuru. . . Kama huduma yangu itadhuriwa na kuihubiri ile kweli, inapaswa kudhuriwa." Hiyo ni kweli.

Akasema, "Utawakasirisha watu nao hawatakupa chochote."

Nikasema, "Sikuwaomba chochote." Nikasema, "Jambo ni kwamba, ya kwamba kwenye Siku ya Hukumu, hapo ndipo itanibidi kujibu."

91 Sikiliza dada, kulikuwa na mwanamke mmoja tu katika Biblia aliyewahi kupaka rangi uso wake, wala hakuupaka rangi apate kukutana na Mungu, aliupaka rangi akakutane na wanaume, na jina lake lilikuwa ni Yezebeli. Hiyo ni kweli. Mnajua yale Mungu aliyomfanyia? Alimlisha kwa mbwa. Kwa hiyo ukimwona mwanamke amejipaka rangi kwelikweli, unaweza kusema, "U hali gani, Binti Nyama Mbwa?" Hivyo ndivyo alivyo hasa mbele za Bwana. Hiyo ni kweli kabisa.

"Vema," unasema, "wanawake wengine hufanya hivyo."

92 Lakini kama wewe ni mwana-kondoo, achilia haki zako! Mungu anakutaka uishi kama mwanamke anavyopaswa kuishi, kama vile mama wa heshima anavyopaswa kuishi. Inakuwa ninii sana. . .

93 Wakati wa vita, nilipanda juu, nilikuwa mlinzi wa wanyama pori, nilikuwa nikipanda juu msituni, na kulikuwako, kule nyuma aliketi mtu fulani, alikuwa mchomelea vyuma. Nami ningeninii. . . Mizaha michafu kuliko yote niliyowahi kusikia, hata ni—niliona aibu kuketi pale na kundi la watu. Na kwa hiyo, jamaa huyu akanitazama, akasema, "Huko nje kuna baridi?"

Nami nikasema, "Naam, ni baridi."

Kasema, "Wewe ni mlinzi wa wanyama."

94 Nikasema, "Naam bwana, naam." Ndipo nikaja kugundua, hapo kando aliketi mwanamke mchomelea vyuma, amevaa ovaroli, zilizojaa grisi, miwani mikubwa juu yake, mkali, anakunywa pombe kama mwanamume, anavuta sigara kama mwanamume, anatukana kama mwanamume. Mungu hakusudii jambo hilo kuwa hivyo. Mungu anataka mwanamke. . .

95 Mungu alipomwumba mtu kwanza, alimwumba mwanamume na mwanamke katika roho; alimfanya katika

mfano Wake Mwenyewe, naye Mungu ni Roho. Wakati alipomtenganisha na kumweka katika mwili, Yeye aliweka roho ya kiume katika mwanamume, na roho ya kike katika mwanamke, na kama kuna jambo lolote kinyume na hilo, kuna upotovu kidogo mle. Kweli kabisa.

96 Ukimwona mwanamke akijaribu kutenda kama mwanamume, kuna kasoro fulani kidogo hapo, seli imechanganyikana mahali fulani. Hiyo ni kweli. Ukimwona mwanamume amekuwa dondoadume sana hata hatahubiri dhidi ya dhambi au kitu kingine kama hicho, kuumiza hisia za mtu fulani, kuna mchanganyiko hapo mahali fulani, pia, si kuzaliwa kwake tu kwa kawaida, bali kuzaliwa kiroho. Loo, tunachohitaji siku hizi ni kwamba mwanamume awe mwanamume, mwanamke, mama wa heshima. Mungu anawakusudia wawe hivyo, wavalie tofauti.

Unasema, "Unatushambulia sisi wanawake."

97 Sasa nitawaambia kuhusu wanaume. Mwanamume yeyote atakayemruhusu mke wake kuvuta sigara, na kuvaa hizo kaptura, na kutenda namna hiyo, kuna *uanaume* kidogo sana ndani yake, nionavyo mimi. Hiyo ni kweli. Nina maoni yangu juu ya mwanamume ambaye atamwacha mkewe afanye hivyo, hakika ni—ninayo.

"Vema, kuna nini?" mnasema.

98 Vema, ndugu, jambo ndilo hili: Mwanamume hapimwi kwa nguvu *hivi*.

"Loo," unasema, "jamaa huyo ni *mwanamume*, ana urefu wa futi sita, ana misuli mikubwa *hivyo*."

99 Nimeona wengi wao wenye uzito wa ratili mia mbili, urefu wa futi sita na nusu, hawakuwa na hata wakia moja ya *mwanamume* ndani yao, wakimtupa mtoto mchanga kutoka mikononi mwa mama na kumbaka huyo mama.

100 Mwanaume hapimwi. . .Huo ni unyama, huo ni unyama, ndivyo nguvu zilivyo. Mwanaume hupimwa kwa tabia. Kamwe hapajakuwapo na mwanaume kama Yesu Kristo, kamwe Yeye hajawahi kufikiwa. Nayo Biblia ilisema, "Hakuwa na uzuri hata tumtamani." Hakuonekana kama Mfalme, Yeye alikuwa ni Jamaa mdogo, labda aliyeinama, mdogo, mdogo wa kimo, bali hakukuwahi kuwapo na mwanaume kama Yeye. Mwanaume hupimwa kwa tabia, si kwa nguvu za kinyama.

Vema, unasema, "Ndugu Branham, hao wengine hufanya hivyo."

101 Sijali yale hao wengine wafanyayo, kama una hiyo nyongo ya uchungu ndani yako, kuna kasoro mahali fulani, kama unaweza kuuvumilia ulimwengu na bado useme kwamba wewe ni Mkristo, kuna kasoro mahali fulani!

102 Nilikuwa tu nikila chakula cha jioni, kulikuwa na jamaa wawili wameketi pale, wahudumu, ukosi uliopinduliwa nyuma, nao wakaketi pale na kunywa michapalo mitatu au minne, mimi na mke wangu, na familia tuliketi pale tukawaangalia, wakafanyiana maskini mizaha michache michafu, wakamaliza kula, kisha wakatoa msokoto mkubwa mno kama, ulionekana kama maksai wa Texas aliyeng'olewa pembe, wameketi pale wakivuta kitu hicho.

103 Unataka kuniambia ya kwamba Hua angemwongoza huyo? La, bwana. Hua Huyo ni mtakatifu. Haleluya! Amewekwa katika Mafuta matakatifu. Huenda mbuzi akafanya hivyo, bali si mwana-kondoo. Tunda la Roho, hilo si tunda la Roho.

104 Watu huenda kwenye roki, kucheza dansi, YMCA yetu wanaiunga mkono, na kufundisha roki. Mengi ya makundi yetu ya kanisa huchukua orofa ya chini, ama kitu kama hiki, chumba cha burudani, na kuwafundisha watu wao roki, huku kitu hicho kimezaliwa kuzimuni, ni ngoma ya Kiafrika.

105 Kupaka uso rangi ni sifa pambanuzi za kipagani. Huko Afrika, mimi ni mmishenari, hao watu huko nyuma ambao kamwe hawakujua mkono wa kulia wala wa kushoto, waangalie hao wanawake jinsi wanavyojipaka matope na kila kitu, ni kweli kabisa, ni ukafiri, ni ibilisi, na inanyemelea makanisani mwetu, nasi basi tunajiita wana-kondoo wa Mungu. Nawaambieni! Tunahitaji kumpata Hua tena.

Sasa, mnasema, "Vema, hilo ni kosa." Ukihubiri hilo kanisani mwako baadhi yao watasema, "Loo, kamwe si—sitarudi tena."

106 Ukikoroma kama mbwa mwitu, mwana-kondoo hufanya nini? Hua hufanya nini, kama ukikoroma kama mbwa mwitu? Anaruka anaenda zake.

"Sitasikiliza hayo tena. Mchungaji wangu anakuwa ninii sana . . . "

107 Vema, hua anaruka mara moja. Hiyo ni kweli kabisa. Yeye hatakaa mahali ambapo ulimwengu umechanganyiwa, kwa sababu Yeye hawezi kuvumilia harufu yake. Hawezi kuuvumilia, hawezi kuula, hawezi kuustahimili. Basi unapoanza kuchanganyikana na ulimwengu, basi Hua anaruka anaenda zake.

108 Na wakati makanisa yanapoanza kusema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Yote hayo hayana budi kuwa ni kitu cha kiakili. Huyo ni ibilisi akifanya miujiza hiyo na kufanya ishara hizo. Ni ya ibilisi," kumbukeni tu sasa hivi, Hua anaruka anaenda zake, kwa kuwa Hua hula Chakula cha Hua. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." [Sehemu tupu kwenye kanda.]

109 "Hiyo ni haki yangu mwenyewe ya Marekani kufanya nitakavyo. Kama nikitaka kinywaji kidogo cha kijamii pamoja na jirani, kama nikitaka kwenda kwenye *hiki*, na kufanya *vile*, hiyo ni haki yangu mwenyewe."

110 Hiyo ni kweli, ni haki yako. Sasa, kama umezaliwa tu kwa roho ya kitaifa utaendelea kufanya hivyo, kama umezaliwa kwa Roho ya Mbinguni hutafanya hivyo tena. Hiyo ni kweli. Kama kanisa linamaanisha tu dhehebu kwako utaishi moja kwa moja kanisani, na kuendelea vivyo hivyo, na kulivumilia, lakini kama wewe ni asili ya Mwana-kondoo, huwezi kulivumilia.

111 Hivi ungeweza kuwazia...? Ninamwona mwana-kondoo huko nje kondeni, akila alfalfa, naye yuko huko nje akila alfalfa, huyu hapa ngu—nguruwe *hapa*, akila mzoga wa farasi. Ungeweza kuwazia hu—huyo nguruwe akisema, "Njoo huku, Bw. Mwana-kondoo, na ule kidogo pamoja nami"? Mbona, mwana-kondoo asingeweza kufanya hivyo hata iweje!

112 Sasa, siwalaumu wenye dhambi kwa kufanya mambo hayo, wao ni nguruwe, kwa vyovyote vile, hilo si kitu, ninawaacha tu waendelee. Ukiwaona huko chini wakinywa pombe, na kufanya yasiyofaa, na kulaani, kufanya mizaha michafu, na mambo machafu, na kutenda kilimwengu, na kusema, "Siamini katika kitu kama uponyaji wa Kiungu." Vema, hakika, hilo ni sawa, yeye ni nguruwe tu, kwa vyovyote vile, si ajabu kumwona juu ya mzoga wa kale, uliokufa, maskini koho.

113 Kinachonishangaza, kumwona mtu anayedai kwamba anampenda Bwana Yesu kisha anafanya jambo kama hilo, kuna kasoro mahali fulani. Kitu fulani kilienda kombo mahali fulani. Kwa sababu kama huyo Hua, kabla Hua huyo hajaingia ndani ya mwana-kondoo huyo, hana budi kuwa ni mwana-kondoo la sivyo Yeye hataingia ndani yake. Huenda akajibunia kitu kama hicho, na kujifanya kwamba yeye ni Mkristo, lakini kama yeye ni Mkristo, atakubaliana na kila Neno ambalo Hua huyo aliandika *Hapa* ndani, ataongozwa na Neno la Mungu.

114 Sasa, tunakoroma na kulipuka, "Huh! Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Nilishuka kwenda kwenye mmoja wa mikutano hiyo ya kale, afadhali ujiepushe na huko, hiyo ni ya ibilisi. Jamaa huyo ni mpiga ramli. Wanawaroga hao watu, hakuna lingine."

115 Huyo ni ibilisi yule yule wa kale aliyesema, "Ni Beelzebuli," ibilisi yule yule wa kale. Anajaribu kukuweka mbali nalo, lijaribu kwa Neno. Mungu hujaribu kila kitu kwa Neno. Chakula cha kondoo ni Neno la Mungu, wana-kondoo Wake hula katika malisho haya mabichi, yenye kivuli.

116 Sasa, tunashangaa siku hizi ni kwa nini hatuwezi kuwa na uamsho. Kwa nini hatuwezi kuwa na uamsho? Kuna nini, hatuwezi kuwa nao? Ni kwa sababu tunafuata uongozi mbaya. Tunaweza kuwa na wongofu wa kujibunia na mikutano

mirefu, lakini inapofikia uamsho halisi, kuna nini? Tunaachilia ulimwengu mwingi sana uingie makanisani mwetu. Ndugu, ninyi wahudumu, mnaamini hilo?

117 Kuna ulimwengu mwingi sana makanisani mwetu. Kama sisi ni Wapentekoste, hebu na tuwe Wapentekoste, na tutende kama Wapentekoste, hebu na tuishi kama Wapentekoste, hebu tuitetee baraka ya Kipentekoste, na tufanye mambo ambayo Pentekoste ilituahidi. Hatuhitaji . . . Pentekoste si dhehebu, Pentekoste ni tukio, hapo ndipo unapofanyika mwana-kondoo, naye Hua anakushika, anaanza kukuongoza. Hapo ndipo sisi ni—ni Pentekoste.

118 Hilo ndilo lililotukia kule juu, wakati Mungu alipomtuma Mwana-kondoo Wake, Naye akafa kwa ajili ya dhambi zetu, na—na ndipo Hua aliposhuka kwenye Siku ya Pentekoste, na kuliongoza Kanisa, Roho Mtakatifu yeye yule aliyeshuka juu ya Mwana-kondoo wa kwanza pale Yordani, Huyo Ndiye yule yule anayeongoza siku hizi.

119 Vema sasa, unapoanza kukoroma, na kusema, "Mimi ni *fulani-wa-fulani*, mimi ni mfuasi wa dhehebu *hili*, hatuamini kitu kama hicho," sasa, Roho Mtakatifu mpole atakulishaje basi? Basi kuna kasoro. Ile . . . Kama . . . Mbuzi angevumilia hilo, bali si kondoo. Kondoo, mwana-kondoo ni mtoto wa Mungu, Roho Mtakatifu huwaongoza watoto wa Mungu.

120 Na leo, tunachohitaji leo ni tukio lingine. Tunachohitaji leo ni kuja tena kwa Hua, na kutua juu ya Kanisa, na kuliongoza, na kuyafungua macho yetu, na kuingia ndani yetu, kusudi tuweze kuona madhihirisho ya Uwepo Wake. Loo, laiti sote tungeweza, kila mmoja hapa ndani aweke tu kando zile hisi za kimbuzi, za mashaka mbali nasi, na kumwacha Hua aingie usiku wa leo!

121 Na wakati Hua, utakapomsikia akipepea aingie moyoni mwako, achukue mahali Pake . . . Hajaenda mbali sana, ameketi tu juu pale kwenye kituo mahali fulani, akikungojea urudi, hakwenda mbali sana, atarudi moja kwa moja.

122 Mnakumbuka wakati tulipokuwa na mikutano ya maombi, miaka mingi iliyopita, na kuomba usiku kucha? Mnakumbuka mikutano hiyo? Mnakumbuka wakati kulikuwako na wale wa mtindo wa kale, nimesikia walivyowaita, watakatifu wanaojibingirisha? Wangeshuka pembeni mwa barabara na kuhubiri na kuomba, na hao akina mama, waliovaa hizo sketi ndefu, wamesimama pale, wakicheza tari, na uso, na nywele zimevutwa nyuma kama kitunguu kilichomenywa.

123 Loo, lakini mnafikiri mmoja wa hawa watazamaji wapya wa *Tunampenda Susie*, angeweza kwenda mtaani namna hiyo? Nasema hawezi. Na halafu kujaribu kusema ati yeye ni mwana-kondoo. Maskini mbuzi wa kale wee! Kuna nini, kwa vyovyote vile? Mnaona? Hiyo ni kweli. Tunachohitaji siku hizi ni wana-

kondoo wengine zaidi wanaoweza kuongozwa, na kula Neno la Mungu.

"Nitavalia nitakavyo, hiyo ni shauri yangu."

La, sivyo, ni shauri ya Mungu.

"Nitaishughulikia familia yangu nitakavyo. Mhubiri hana shughuli kuniambia hivyo."

124 Naam, ninapaswa, pia. Unapaswa kuishughulikia jinsi Mungu alivyokwambia uishughulikie. Hiyo ni kweli, achana na upuuzi huu wote. Lakini hatufanyi hivyo. Mnaona ni kitu gani? Tulilegeza kamba. Nini kilitukia? Roho Mtakatifu aliruka akaenda Zake. Wakati ulipoanza kutenda namna hiyo, Roho Mtakatifu aliondoka. Hiyo ndiyo sababu anaporudi kanisani, unashangaa tu, "Kuna nini?" Unaona? Si—si—si kitu ambacho ninii . . .

Ungesema, "Vema, labda nisingetoka nje na kufanya *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*."

125 Aliye na hatia kwa iliyo ndogo sana ana hatia ya yote. Huna budi kujisalimisha kwa Mungu, na kumwacha Roho Mtakatifu akuongoze.

126 Dhambi ni nini, kwa vyovyote vile? Dhambi ni kutokuamini. "Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa." Hiyo ni kweli. Sisi ni wenye dhambi, kwa sababu sisi si waaminio. Nilikuwa . . . Vema, hao makuhani huko nyuma katika siku hizo ambao Yesu aliwaita wenye dhambi, na majoka, na nyoka nyasini, na baba yao alikuwa ni ibilisi, na kadhalika, watu hao waliishi safi tu walivyoweza kutembea, lakini waliongozwa na kanisa lao. Kama Roho Mtakatifu angalikuwa akiwaongoza, wangemjua Yeye.

127 Akasema, "Kama mngalimjua Baba Yangu, mngalinijua Mimi, kwa vyovyote vile. Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi." Kwa kuwa yu—yule Hua alikuwa ndani Yake, naye Hua alikuwa akifanya dhihirisho. Hili hapa linakuja, iweni tayari: Naye Hua ndani yetu leo hii, atatoa kitu kile kile alichotoa katika Mwana-Kondoo, huduma ile ile, ishara zile zile, maajabu yale yale. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo, Yeye naye atazifanya, zaidi ya hizi atazifanya, maana ninaenda kwa Baba Yangu. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari."

128 Loo, ni thibitisho la jinsi gani kuona mwana-kondoo na Hua wakija pamoja, Mbingu na nchi zimeungana, Mungu na mwanadamu wameungana! Na, mbona, dha—dhambi za ulimwengu ziliondolewa, na—na ukali wote, na mauti yote, na huzuni zote, na magonjwa yote yaliondolewa wakati Mwana-kondoo na Hua walipoungana pamoja. Naye atakufanyia jambo

lile lile, atakapoungana nawe, wakati Hua na mwana-kondoo wanapokutana, tabia zao ni sawa.

129 Sasa, mnaweza kuona ni kwa nini watu wanasema, wahudumu wenye majina makubwa mno ya kikasisi, na kadhalika, ya—ya “Baba Mtukufu,” “Daktari *Nanii*,” kwamba, jinsi wao. . .unasema, “Loo, huo—huo, usiamini upuuzi huo wa uponyaji wa Kiungu, usiamini upuuzi huo wa watakatifu wanaojibingirisha kama hao Wapentekoste, usiuamini huo.”

130 Mnaona, ni mbuzi badala ya mwana-kondoo, mnaona, wanakula kwenye. . .Neno la Mungu, ndilo Chakula cha Mwana-kondoo. Mungu anawaongoza, na jinsi alivyomwongoza yule Mwana-kondoo wa kwanza. . .

131 Vipi kama Yesu angesimama na kusema, “Sasa, ngoja kidogo, Musa alikuwa nabii mkuu, hiyo ni kweli, lakini hizo siku zimepita”?

132 Huyo asingekuwa ni Mwana-kondoo, asingekuwa ni Mwana-kondoo wa Mungu. La, bwana. Daima alithibitisha ya kwamba “Si Mimi nizitendaye hizo kazi, ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu. Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, msiniamini Mimi, bali nikizitenda kazi za Baba Yangu, msiweze kuniamini Mimi, aminini hizo kazi.” Hivyo ndivyo Mwana-kondoo alivyokuwa akiongoza, ilikuwa ni Mungu ndani Yake. Ni Mungu ndani ya Kanisa, ni Mungu ndani ya watu Wake siku hizi, ni Mungu akijidhihirisha Mwenyewe kwa njia ya Roho Mtakatifu akiishi ndani ya Kanisa juu ya wana-kondoo Wake. Unaamini hilo kwa moyo wako wote?

133 Na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu. Hua na Mwana-kondoo. Wakati mkisikiliza, Maandiko yaliyo maarufu sana, mojawapo, ambalo ninaweza kuwazia, wakati Yesu aliposema, “Baba,” wazia hilo, “Baba, kwa ajili yao najitakasa Mwenyewe.” Wazia hilo, “Baba, kwa ajili yao najitakasa Mwenyewe.” Alikuwa akifanya nini? Akiweka mfano, Yeye alikuwa ni Mwana-kondoo.

134 Alifanya nini? Alikuwa na haki ya kuwa na makazi, alikuwa mwanaume; alikuwa na haki ya kuoa, alikuwa mwanaume; Alikuwa na haki ya kuvaa nguo nzuri, alikuwa mwa—mwanaume, bali alijitakasa Mwenyewe, aliachilia. Angeweza—angeweza kushuka kwenye ushoroba wa Utukufuni, mtu mkamilifu pamoja na bendi ya Malaika, hakika, bali Yeye alijitakasa Mwenyewe. Angeweza angalau kuzaliwa katika kitanda kizuri, safi mahali fulani, bali alizaliwa katika hori juu ya lundo la samadi, katika hori la kuazima, bali alijitakasa Mwenyewe. Kwa nini? Alikuwa ni Mwana-kondoo.

135 Mnaona, marafiki, tumerudi kwenye dini za miungano, na kadhalika, na mambo haya yote, tunaondoka kwenye kitu kilicho halisi, jinyenyekeze. Endelea kuwa mnyenyekevu, “Bwana, unitakase.”

136 Yesu alikuwa akiwafundisha watu fulani ambao walikuwa wanaenda kuipeleka Injili ulimwenguni kote, watu kumi na wawili, kwa hiyo aliishi maisha yaliyotakaswa na akaachilia kila anasa ya ulimwengu kwa ajili yao. Tunapaswa kuachilia mavazi yetu ya kilimwengu, na anasa zetu za kilimwengu, na mambo kama hayo, kwa ajili ya watu tunaojaribu kuwaongoza kwa Mungu, ulimwengu wa nje. Jalia Hua aingie usiku wa leo, ujitakase, kusudi Hua wa imani halisi aingie na kufanya makao Yake.

137 Baba yetu wa Mbinguni, ujumbe huu wa *Mwana-kondoo Na Hua,* jinsi impasavyo Mwana-kondoo, jamaa mdogo, asiye na hatia, kuongozwa, yeye hajaribu kutumia mawazo yake mwenyewe, hana budi kuongozwa; alifanywa hivyo kusudi mchungaji aweze kumwongoza.

138 Ee Mungu, ondoa ukubwa wote ndani yetu, ondoa hisia zote za majivuno, na—na za kiburi, na ujuaji, utuondolee, Bwana, mashaka yote na hitilafu ambazo—ambazo zimepenya ndani, ziondoe, Bwana. Jalia Hua ashuke chini usiku wa leo, aingie katika kila moyo, tupate kuachilia haki zetu, huenda tukapoteza mambo yote tunayohisi tuna haki yake kama raia wa Marekani, hebu na tuiachilie, ili Hua apate kutuongoza kwenye amani, na fadhili, na rehema, na utukufu wa Mungu.

139 Baba, ninajisalimisha Kwako usiku wa leo kwa ajili ya ibada hii ya uponyaji inayokuja. Jalia Hua aruke chini, Bwana, jalia aingie moyoni mwangu, na kinywani mwangu, akilini mwangu, machoni mwangu, sauti yangu, na uwajalie huko nje, Bwana, wajue ya kwamba ni Wewe. Jalia aingie ndani yao, na kwa pamoja jalia wailaani dhambi, wayahukumu maradhi, sifa zote za dhambi, jalia zitoweke usiku wa leo.

140 Jalia Kanisa hili litoke hapa usiku wa leo kama Kanisa lililosuguliwa, lililotakaswa, lililojazwa, linaloamini, lililojazwa na Roho Mtakatifu, liondoke tangu usiku huu na kuendelea, Bwana, na uamsho mkuu uanze kote nchini, ambao tunaombea. Jalia tuone watu wamezizunguka madhabahu tena, na mioto ya uamsho ikiwaka, kila kanisa limejaa, mpaka iwabidi kujenga makanisa mapya, vyumba vya shule ya Jumapili vijengwe. Ee Mungu, tujalie usiku wa leo, kabla ya kuja kwa Bwana Yesu, kwa kuwa tunaamini ya kwamba kumekaribia. Na tuachane na kila kitu cha kilimwengu, tupate kumwona Kristo maishani mwetu, tuongozwe na Roho Wake. Tujalie, Bwana.

141 Sasa, najua ujumbe huu mdogo, kidogo umekatakatwa, huku nikiishikilia sauti yangu, nisije nikapwelewa na sauti, ninaomba ya kwamba kwa namna fulani, itashikilia usiku wa leo, kutoka papa hapa mahali hapa, kitu fulani chenye kilindi na imara na kizima, ambapo kila mtu humu ndani atakuwa mzaa matunda, si kujaribu kujibunia chochote, ama kutengeneza chochote, bali wajisalimishe tu kwa Roho Mtakatifu. Na jalia wazae tunda la

imani, na amani, na furaha, na wema, na rehema, na kiasi, na karama zote nzuri za Mungu.

142 Jalia kuingie makanisani, unabii, kunena kwa lugha, tafsiri, maarifa, hekima. Tujalie, Bwana. Jalia kanisa hili kuu la Kipentekoste liinuke na kujitikisa litoke mavumbini, lipitie kwenye zile njia za kale tena, na kuziombea, Bwana, na kupitia mle, maana ndiyo njia nzuri ya kale. Ndiyo njia ya kale ya Injili, ingawa inanenwa vibaya, hata hivyo ndiyo kitu adhimu kuliko vyote kilichoko duniani, kwa sababu Hua ameshuka, akitafuta wana-kondoo ambao angeweza kuwaongoza.

143 Mungu, kama angeweza kuachilia Maisha Yake Mwenyewe ya thamani, ajitolee kwenda msalabani kama Kijana na kufa kwa ajili yetu, "Si mapenzi Yangu, bali Yako yatendeke," Mungu, hakika, kufurahia wokovu Wake, kufurahia Uzima wa Milele katika nyakati zijazo, hakika, tunaweza kuachilia dhambi zetu na mambo yetu ya ulimwengu, tupate kuona kile Yeye alichokufia, yule Mwana-kondoo wa thamani wa Mungu.

144 Tujalie usiku wa leo, Bwana, huku umetia nanga kwa utulivu na kwa uchaji katika kila moyo. Ninayakabidhi yote Kwako, Bwana, tunapowaita watoto Wako wagonjwa kuomba. Hebu mapigo yaliyo juu ya Mwana-kondoo huyo, usiku wa leo, yamponye kila mwana-kondoo anayeingia mstarini, ama, aliye humu jengoni. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

145 Ninapenda utamu wa Roho Mtakatifu, nanyi je? Una—unazama tu ndani yangu sana. Kuwazia juu ya. . . Kuangalia nyuma kwenye shimo nilimotoka, kuangalia nyuma. . . Ninachukia kuhukumu dhambi kama nifanyavyo, mimi—mimi, wakati mwingine silimaanishi kibinafsi, bali kama mhudumu, mimi—mimi, ofisi yangu maishani, si—sina budi kuihukumu, enyi marafiki, si—siwezi kujizuia. Simaanishi kumwudhi mtu yeyote, bali ninakusudia kuihukumu. Naam. Lakini ninawatakeni mjue ni kwa utamu kutoka moyoni mwangu, Mungu anajua hilo.

146 Hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikifanya mkutano mjini, nikaingia mahali fulani. Tulikuwa tukila ng'ambo ya barabara katika mkahawa mdogo wa Dunkard, ilikuwa huko juu mahali fulani huko Ohio. Mpenzi, unakumbuka ilikuwa wapi? Ninasahau, ilikuwa mahali fulani huko Ohio, kule, tulikuwa katika jengo kubwa la ghala la silaha, nalo lilikuwa limejaa, na maelfu ya watu.

147 Waliniweka nje mashambani, maana kulikuwa na wengi sana huko chini waliojua mahali nilipokuwa ninaishi. Basi, tukaenda mashambani na tulikuwa, tukila ngambo ya pili, Mkahawa mdogo wa Dunkard, maskini wasichana wazuri sana, safi, wakitembea pale, na wazuri sana na kila kitu.

148 Na kwa hiyo basi, Jumapili, walifunga wakaenda kanisani, nami sikuwa nimekula kwa siku mbili, kwa hiyo ilinibidi

kuhubiri alasiri hiyo, nikavuka kwenda kwenye mkahawa mdogo wa kisasa, ng'ambo ya barabara, ama, upande wa pili wa barabara ambapo barabara kuu zinakingamana, basi nikaenda kule, ndipo nilipoingia mle, ilikuwa ni jambo la aibu. Huku amesimama akicheza mtambo wa karata, alikuwa ni a—afisa, afisa wa polisi, yapata umri wangu, mnajua ameoa, huku amemkumbatia mwanamke kwa utovu wa uadilifu, akicheza mtambo wa karata, huku kucheza kamari ni haramu huko Ohio. Haya basi.

149 Nikaangalia huko nyuma, na hapo wameketi, baadhi ya hawa waliojifanya Elvis Presley, pamoja na hawa, kama bata aliyeketi nyuma ya kichwa chao, na—na upuuzi huo wote wa namna hiyo, majambazi huku suruali zao zimevutwa chini namna *hii*, nao wameketi pale na msichana mdogo mikononi mwao. Kamwe nisingeweza kulisema katika kusanyiko lililochanganyikana.

150 Nikamwangalia ameketi mkono wa kulia, hapo aliketi mwanamke mkongwe, mwenye umri mkubwa wa kutosha kuwa nyanya yangu, karibu hivyo, ameketi pale na amejipaka kitu hicho cha zambarau midomoni mwake, na kucha zake za miguu zimepakwa rangi vivyo hivyo, amevaa maskini jozi ya nguo hizi ndogo, za kizinifu, na maskini, kizee, ngozi yake inaning'inia chini namna *hii* mikononi mwake, naye ameketi pale akiwa na madoa madogo ya samawati usoni mwake namna *hii* mahali alipokuwa amezipaka rangi, pamoja na nywele zilizopakwa rangi ya samawati.

Ndipo nikaangalia, nikawaza, "Loo, jamani!"

151 Huku wazee wawili wameketi pale, na ni majira ya kiangazi, mmoja wao amevaa kabuti kubwa la jeshi, skafu imening'inia chini namna *hii*, ameketi pale pamoja na maskini huyo mama mkongwe, na bia imewekwa pale, wakinywa. Ndipo mmoja wao akamtazama huyo mwingine, na kusema, "Unafikiri mvua itadhuru rubabu?" Nao wakaomba radhi wakaenda msalani.

152 Ndipo nikasimama pale, nikasema, "Mungu, Wewe katika utakatifu Wako, ungewezaje kamwe kusimama kuliangalia hilo wakati linaniua kuliangalia?" Nikasema, "Mbona, usikipige kitu hicho kiondoke duniani? Usikiache hapa tena." Nikasema, "Maskini Sarah na Rebekah wangu," huko, "itawalazimu kulelewa katika mazingira kama hayo?" Nikasema, "Mungu kiangamize kutoka duniani! Wewe ni mtakatifu, unawezaje kufanya hivyo?"

Kitu fulani kikaniambia, "Ingia nyuma ya mlango."

153 Nikarudi nyuma ya mlango na kusimama pale. Nikangojea kidogo, ono likaja, nikaona dunia ikizunguka. Na kote kuizunguka dunia kulikuwa na ukungu ulioonekana kama Damu, ukirashia kila mahali. Nami nikaangalia mle ndani, nami huyo hapo nikifanya mambo mabaya. Basi kila wakati

ningefanya jambo baya, dhambi zangu zingeenda mbele za Mungu, naye Mungu angeliniua kwa ajili yake, bali Yesu alikuwa amesimama pale kama bamba, akaishika, ningeona machozi yakitiririka mashavuni Mwake. Kisha ningefanya jambo lingine baya, Damu Yake ingelishika, lisije—lisije likanigusa, lisiniue, Mungu angeniua, Yeye, "Siku utakayokula, ndiyo siku utakayokufa."

154 Nami nikaitazama, na katika hilo ono nikamwendea, nikasema, "Bwana, ninajionea aibu." Hicho hapo kitabu changu kimewekwa pale na kila namna ya uovu umeandikwa juu yake. Nikasema, "Je, utanisamehe, Bwana? Hivi nilikuweka katika hali hiyo? Hivi dhambi zangu zilikufanya ufe kwa ajili yangu? Ee Mwana-kondoo, naomba unisamehe dhambi zangu, sitafanya hivyo tena."

155 Akanyosha mkono nyuma, akautikisa mkono Wake *hivi*, na kuandika kote kitabuni kwa Damu Yake Mwenyewe, "Amesamehewa," akakitupa nyuma Yake, ndiposa akafanya hivyo, akafungua kitabu kipya.

Nikasema, "Asante, Bwana. Nitafanya lolote unaloniambia nifanye. Nakupenda, Bwana Yesu."

156 Akasema, "Sasa, nimekusamehe bure kwa yote uliyofanya," kisha akageuka, nikamwona mwanamke huyo, kasema, "lakini ulitaka kumwondoa juu ya uso wa nchi."

Loo, nilijisikia kuwa mkubwa *hivyo*. Nikasema, "Nisamehe, Bwana."

157 Wakati lile ono liliponiacha nilitoka nikaenda kwenye ile meza ndogo alipokuwa, nami nikasema, "U hali gani?"

Naye akainua macho yake, alikuwa amelewa-nusu, akashikwa na kwikwi mara kadhaa, akasema, "Loo, aloo."

Na—nami nikasema, "Naweza kuketi?"

Akasema, "Asante, nina wenzangu."

Nikasema, "Sikulimaanisha hivyo. Ningependa tu kukwambia neno moja."

Naye akasema, "Endelea uliseme."

158 Nami nikaketi chini, nikasema, "Umekuwa ukiishi maisha haya kwa muda gani?" Akaniangalia, na maskini, mzee, nami ni—nikawazia, "Jamani, haidhuru nini, vipi, yale aliyopitia!" Basi nikamwambia kilichotukia. Nikasema, "Samahani."

Akasema, "Je, wewe ni yule mhudumu hapa chini, Bw. Branham, ambaye huu . . .?"

Nikasema, "Naam."

159 Akanyosha mkono na kuushika mkono wangu, akitetemeka, akaanza kulia, akasema, "Bwana," akasema, "mume wangu alikuwa mhubiri." Akasema, "Baada ya kifo chake . . . Ninao wasichana wawili, hao ni walimu wa shule ya Jumapili, wote

wawili." Naye akanisimulia hiyo hadithi, kile kilichotukia, jinsi alivyokuwa akiishi. Akasema, "Nimevuka mpaka wa matumaini."

Nikasema, "La, hujavuka. La, hujavuka."

Akasema, "Na—nataka kujiweka sawa." Lakini akasema, "Sina mahali pa kuanzia."

160 Nikasema, "Ati nini? Sasa hivi. Huku Mungu akinionyesha nyuma ya mlango lile ono pale, mimi nikitaka kukuangamiza, Naye akasema amenisamehe, nami ninataka kukuhukumu, mama, nisamehe."

161 Hapo akaishika mikono yangu, nikamwongoza moja kwa moja huko nje amevaa maskini hizo kaptura, moja kwa moja katikati ya sakafu hiyo namna hiyo, nasi tukapiga magoti, ndipo tukawa na mkutano halisi wa maombi pale. Nilipomaliza, watu walikuwa wakilia, wakitembea pale.

162 Nawaambia, ndugu, wakati mwingine inatubidi kunena dhidi ya dhambi, sio kumwudhi huyo mtu, ni kuwaleta wapate kutambua, kuwaleta mahali pa kutambua. Kama vile Bwana wetu, hatumaanishi kuudhi ama kuwa wabaya, Mungu anajua hilo. Hilo halingeninii, hilo . . . Kamwe hilo lisiwe nafsini mwangu, bali ni kujaribu kuwafanya watu watambue kinachoendelea, kinachotendeka. Mnaona? Nami ninafanya hivi ili kwamba tutaacha kutokuamini kwote, na mambo ya ulimwengu, na kurudi, na kuwa Mkristo halisi, mwema, mnyenyekevu, na kumwishia Yeye.

163 Sasa, Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamtuma Hua usiku wa leo, na kutuongoza sote katika hilo, kwa utulivu na utamu, hadi mahali hapo halisi. Eliya alilala pangoni, na ndani ya pango hilo upepo ukapita, radi ikamulika, ngurumo zikanguruma, nchi ikatetemeka, lakini Sauti ndogo tulivu ndiyo iliyomvutia huyo nabii.

164 Mungu, tujalie usiku wa leo, sisi . . . kila kitu kimepita, jalia hiyo Sauti ndogo tulivu iwavutie watu usiku wa leo kwenye maisha halisi, yaliyotakaswa, maisha ambayo yatamtetea Mungu wao, yatakayolitetea kanisa lao, yatakayomtetea mchungaji wao, yatakayoitetea huduma ya Kristo, yatakayoinua bendera, ambayo yataishi, yatende, yavae, yaende, na kushirikiana, na kuishi katika hayo mazingira, ambayo yatakolea chumvi sana, ambayo yatawafanya wengine kuona kiu kuwa kama wao. Tujalie, Bwana.

165 Jalia kanisa letu lisichafuliwe sana hata lionekane kama walimwengu wengine, ambapo huwezi kutofautisha mwenye dhambi na mtakatifu. Mungu, jalia kwamba litakuwa halisi. Lifanye halisi, Baba, ninaomba, ninapokuomba Wewe utusaidie, usiku wa leo, na kutangaza ya kwamba Wewe upo hapa kuunga mkono mambo haya, katika Jina la Yesu, Mwanao.

166 Wakati tumeinamisha vichwa vyetu, kuna mtu yeyote humu jengoni usiku wa leo, ama ni wangapi, niseme, wangetaka kuishi hayo—kuishi hayo maisha halisi, ya amani na matamu, na kuongozwa na Mwana-kondoo, ama, na Hua? Mimi si, ninataka kila mtu ainamishe kichwa chake na kila jicho lifumbwe, sitafanya wito wa madhabahuni, ninataka tu kuijua mioyo yenu. Inua mkono wako, useme... Mungu akubariki. Loo, hilo... Angalieni kote jengoni kila mahali, hakika, kila mahali, hakika, mnaona.

167 Baba wa Mbinguni, tujalie, tafadhali utujalie, Mungu. Kuna wengi hapa, kama nikirudi mwaka mmoja kuanzia leo, hawatakuwa hapa, Huenda nisiwe hapa pia, Bwana, mwaka mmoja kuanzia leo. Sina budi kukutana Nawe mbele yao wote siku moja. Na kulingana na ono hilo ulilonionyesha hivi majuzi, Bwana, ninataka kila pembe niwezayo kumleta mtu fulani.

168 Wape shauku ya moyo wao usiku wa leo. Jalia Hua wa Mungu atuongoze kwenye vilindi virefu zaidi na juu zaidi kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

169 Sasa, ninaamini mwanangu aliniambia muda mfupi uliopita nikiingia, tulipokutana naye huko nje, kwamba alikuwa na kadi hamsini za maombi zilizopangwa usiku wa leo, alizowapa watu. Tutawaweka kwenye mstari na kuwaombea. Nilisahau, ipi...? [Ndugu Billy Paul anasema, "C."—Mh.] C, Billy, sikukuona... C, moja hadi hamsini. Sasa, tunaleta hizi... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

170 ...maskini mwanamke huyo amevaa nguo yenye milia, ni—ni—ni sehemu gani ya...? Kutoka mahali fulani huko chini kusini. Kama mkiliwazia wakati nikilisimulia, nikumbusheni...

171 Mvua ilikuwa inanyesha sana, na—na mahali hapo palikuwa pamejaa, nao walikuwa wamesimama kando ya kuta. Na kwa hiyo, wao... Ilikuwa... Billy alikuwa amegawa kadi za maombi, halafu basi, pia kulikuwa na maskini mama mmoja akitembea huku na huko, alikuwa amemfunika mtoto mchanga kwa blanketi. Pia kulikuwako na maskini—maskini mwanamke mwingine mkongwe ameketi pale amevaa moja ya hizo nguo ndogo za ging'am, ama chochote kile, mwajua, ameketi pale, maskini Mkristo mtakatifu, ameketi mbele. Naye alikuwa, mama huyu hakuwa na mahali pa ku—ku—kuketi pamoja na mtoto mchanga. Ndipo maskini mama huyu akaanza kumhurumia mtoto huyo mchanga na maskini mwanamke huyo akitembea huku na huko, ndipo Roho Mtakatifu akamwambia huyo mama, "Mwombee mtoto huyo."

"Loo," akasema, "nisingeweza kumwomba mwanamke huyo."

"Mwombee huyo mtoto."

172 "Loo, mimi—mimi..." Ni bora kufanya yale Mungu anayokwambia ufanye. Na kwa hiyo, wakati yeye...Akasema, "Vema, wakati mwingine atakapopitia hapa, nitamwuliza kama ninaweza kumwombea mtoto huyo."

173 Basi alipopitia hapo alikuwa amebeba kadi ya maombi. "Loo," akasema, "nisingemwomba nimwombee mtoto huyo mchanga, mbona, Ndugu Branham atamwombea mtoto huyo." Kana kwamba hilo lilimaanisha zaidi ya chochote, mtu mwingine yeyote. Kasema, "Ndugu Branham atamwombea mtoto huyo mchanga."

174 Kwa hiyo Roho Mtakatifu akaendelea kushughulika naye, nao wakati ukaendelea. Sikuwa nimekuja bado, na kwa hiyo basi, maskini huyo mwanamke akasema, vema, akashawishika sana, kasema, "Dada, ungetaka kuketi chini pamoja na huyo mtoto mchanga?"

"Loo," akasema, "sitaki kuchukua kiti chako, mpenzi."

175 Na labda huruma ya maskini mama huyo, ilikuwa ni zaidi kwa mtoto huyo mchanga kuliko vile yangu ingalikuwa. Basi akasema, "Dada," kasema, "chukua kiti hiki uketi. Lakini," kasema, "ninataka kukwambia, najua wewe ni Mkristo."

Akasema, "Naam, mama, ndivyo nilivyo."

176 Naye akasema, "Mimi pia ni Mkristo." Kasema, "Mungu aliendelea tu kusema nami, 'Mwombee mtoto huyo.'" Kasema, "Unayo kadi hapo." Kasema, "Ndugu Branham atamwombea mtoto huyo mchanga."

177 Akasema, "Natumaini ataita namba yangu usiku wa leo. Niko hapa kuombewa, pamoja na mtoto wangu mchanga," kisha kasema, "ni mahututi." Basi—basi kasema, "Natumaini ataita namba yangu."

178 Naye akasema, "Vema, wewe keti hapa chini, na uniache nimwombee mtoto huyu, ili niweze tu kuliondoa moyoni mwangu," kasema, "kwa sababu ninajisikia kuhukumiwa nisipofanya hivyo."

Akasema, "Mbona, bila shaka, mpenzi, wewe mwombee mtoto."

179 Naye akaomba ombi dogo, akakaa, akasema, "Bwana Yesu, ulikuwa ukiuonya moyo wangu, nami nikamwekea tu mikono huyu mtoto mchanga. Na kama nimekosea wakati mtumishi Wako atamwombea, usi—usiache liakisi, Bwana, Ni—ninajaribu tu kutuliza hisia zangu." Huyo ni Roho Mtakatifu akimwambia maskini huyo mwanamke hivyo.

180 Kwa hiyo akamwombea huyo mtoto mchanga, kisha huyo mwanamke akampa huyo mama mwenye kadi ya maombi na mtoto hicho kiti, ndipo maskini mama huyo akapanda juu na kusimama huko juu kabisa kwenye roshani.

181 Vema, baada ya kitambo kidogo, mvua ikapungua kidogo, nami nikaingia, nikaingia, nikaenda jukwaani, nikahubiri kwa muda kidogo, nikaitisha mstari wa maombi, nami nikaita tu yapata kadi kumi, ama kitu kama hicho, maana yote yalipaswa kuwa katika upambanuzi. Na wakati mwingine kwa njia hiyo, ninapofikia kumi, ni—niko karibu sana kwisha kama ni mkutano mpya. Kwa hiyo basi, wakati wao—wao. . . Nikawaambia, nikasema, "Sasa, enyi marafiki, ninyi, ni imani yako, huna budi kuamini. Mimi. . . "

182 Kwa hiyo wakati—wakati walipoita namba hiyo, ninaamini, kuanzia, kama kutoka ishirini hadi thelathini, ama kitu kama hicho, ama thelathini hadi arobaini, zozote zile, maskini mwanamke huyo alikuwa kama wa nne mstarini pamoja na mtoto huyo mchanga. Maskini huyo mama alijisikia vizuri sana wakati huo. Kwa hiyo huyo mtoto mchanga na mama yake wakaja, na maskini huyo mtoto alikuwa amefunikwa kwa blanketi, namna *hii*, naye alikuwa mahututi.

183 Kwa hiyo, ikafikia mahali ambapo mstari wa maombi ulikuwa ukiendelea, alipokaribia, nikasema, "U hali gani?" Nililipata kwenye kanda, mnaona, hivyo ndivyo nilivyojua yote kulihusu. Kwa hiyo nikasema, "U hali gani?"

Naye akasema, "U hali gani?"

Nikasema, "Nadhani hatufahamiani?" Nilikuwa nikijaribu kuwasiliana na roho yake wakati huo, mnaona.

Naye akasema, "Naam, bwana, hatufahamiani."

Nikasema, "Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe, ni kwa ajili ya mtoto wako mchanga."

Akasema, "Hiyo ni kweli."

Nikasema, "Ana lukemia."

Naye akasema, "Hiyo ni kweli. Madaktari wamempa miezi michache tu ya kuishi."

184 Nikasema, "Vema, ngoja kidogo," nikasema, "huyo mtoto tayari ameponywa. Kuna maskini mwanamke mmoja ambaye ndio kwanza amwombee ambaye amevaa ma—maskini nguo ya ging'amu." Nikasema, "Yeye ndio kwanza amwombee huyo mtoto dakika chache zilizopita." Nikasema, "Huyo ni yeye anayesimama moja kwa moja pale juu, jina lake ni Bibi *Nanii*, na *nanii*." Yeye. . . Basi kutii ni bora kuliko dhabihu.

185 Sasa, Roho yuyo huyo aliyewashuhudia usiku wa leo, "Mimi ni Hua, nipo hapa, wewe ni mwana-kondoo Wangu, ninataka kukuponya."

Mbona, sema tu, "Asante, Baba wa Mbinguni." Uondoke moja kwa moja umeponywa. Hivyo ndivyo inavyofanywa.

186 Vema, hebu tuitishe mstari wa maombi. Ninaendelea tu kuzungumza, ninyi ni wasikilizaji wazuri sana na mnaketi

kimakini sana, Kweli ninathamini hilo. Sasa, hebu tuone, kadi ya maombi . . . Vema, hebu tuwalete wote huku, nasi tutawaombea tu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

187 . . . Roho Mtakatifu anaweza tu kushikilia. Mnajitahidi sana, najua mnajitahidi, mnaona, mnajaribu kujipenyeza ndani yake, lakini kama mngeweza tu, msijaribu kujipenyeza, jiachilieni tu, mwacheni tu Mungu alifanye. Bila shaka litakuwa—bila shaka litakuwa ni jambo zuri sana kama tu mtamruhusu Mungu afanye hivyo, hakutakuwako na mgonjwa atakayesalia miongoni mwetu. Sasa, kama ninyi nyote sasa mtaamini kwa moyo wenu wote, kwa nguvu zenu zote, Mungu atawajalia uponyaji wenu, mnaona. Mnaamini hilo?

188 Na—na—naamini tayari inatendeka. Loo, laiti ingaliendelea tu! Kabla mtu yeyote hajapata kuingia kwenye mstari wa maombi, niliona Nuru hiyo ikifanya duara moja kwa moja namna *hiyo*, wakati uo huo tu. Nilikuwa nikiiangalia nione kama ilisimama juu ya mtu fulani, ikasogea *hivi* upande *huu*. Sasa iweni tu na imani.

189 Sasa, ni wangapi wameiona picha ya Malaika wa Bwana hapa? Tu—tunayo humu ndani, iko kwenye vitabu, na kadhalika. Sasa, hiyo ndiyo niliyokuwa nikiangalia wakati huo tu, ilitokea *kule* mahali fulani, ikazunguka *hivi*, ikaja upande *huu*.

190 Daima huja kwenye mstari wa maombi, daima imekuja, mkono wangu wa kulia, hiyo ndiyo sababu ninawaleta watu hivyo. Kamwe sifanyi mstari wa maombi isipokuwa utokee kwenye mkono wangu wa kulia, ukija kushoto, maana sikuzote hapo ndipo anaposimama, hapo ndipo sikuzote ninapomwona, upande huo. Na sasa, wakati ilipokuwa, niliwaleta watu kutoka mkono wa kushoto, nilipowashika kwa mkono huo, lakini upande huu ni ono, Yeye husimama upande huu. Vema.

191 Sasa, ndugu wahudumu, ninawatakeni nyote kuamini kwa moyo wenu wote. Ninawatakeni mwe na imani, na muwaangalie watu hao.

192 Sasa, je, Mungu ni Baba? Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Mungu ni Baba yetu? Ni Baba wa Yesu Kristo, na Ndiye Baba yetu, sisi ni watoto waliofanywa wana wenye mamlaka. Sasa, Yeye ni Hua. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba kwa neema ya Mungu, wewe ni mwana-kondoo Wake? Inua mkono wako. Sawa. Vema. Sasa hebu na tumruhusu Yeye atuongoze. Sasa, nitaninii, ninataka kuona katika kusanyiko, mtu fulani kusudi mpate kuona sio hawa watu hapa mstarini tu, wanaoninii tu, wanaoninii . . .

193 Mnajua ni kwa nini sisi hugawa kadi za maombi? Ni kusudi watu wasikimbie. Mnaona, kuna—labda kuna watu mia mbili au mia tatu zaidi, ama nne, hapa wanaotaka kuombewa. Na kama una upambanuzi, ndugu, wao, ni kurukiana, na machafuko. Huu—huu ni—*ni* uwanja wa michezo, lakini sivyo ulivyo usiku

wa leo, ni kanisa usiku wa leo, Kanisa la Mungu limeketi humu ndani. Kwa hiyo, tunataka kila kitu katika utaratibu.

194 Hebu kivurugike, mkaangalie jinsi Roho Mtakatifu atakavyoondoka upesi. Loo, ni mwoga kweli! Hebu mtu fulani aanze kutokuamini, angalieni tu jinsi inavyoniacha, u—upesi tu iwezavyo. Haitakaa, kamwe haitakaa mahali palipo na kutokuamini, kweli haitakaa, ni mwoga sana, sana. Hiyo ndiyo sababu, ndugu yangu . . .

195 Dada zangu wa thamani, Mungu aubariki moyo wako, mimi nikizungumza kuhusu kuvalia kwa wanawake, hao—hao si ninyi, hao ni hawa wa kisasa wanaofanya jinsi wanavyofanya. Lakini angalieni, ninajaribu tu kuwaonya, kwa ajili ya watoto wenu wanaokuja, na kadhalika, na—na angalieni kila hatua, msifanye hivyo.

196 Jana usiku niliona upande *huu*, na upande *ule*, wasichana matineja, wasichana, wakirudi sasa kwa ajili ya wokovu. Jinsi ninavyothamini hilo! Jamani, moja kwa moja kwenye hizo njia panda za maisha. Jinsi lilivyo na neema, Mungu angefanya hivyo kwa ajili yetu!

197 Sasa, ni . . .? Je, wote waliingia? Je, wale hamsini wote wapo? Kuna mtu fulani mahali fulani anayejaribu kuamini huko nje, mahali fulani. Inaninii tu . . . Mimi . . . Hakuna haja . . . Kama niliwaambia ningeweza kuelezea jambo hili, hamwezi. Ni wangapi wanaojua hilo? Huwezi kumfafanua Mungu. Hiyo ndiyo sababu majaribu yetu yote na ushirikina . . .

198 Katika bustani ya Edeni kulikuwa na miti miwili. Ni wangapi wanaojua hilo? Mmoja wao ulikuwa ni ule Mti wa Uzima, na huo mwingine ulikuwa ni Mti wa Maarifa. Basi mwanadamu alipouacha Mti wa Uzima apate kula Mti wa Maarifa, sikuzote hujiangamiza mwenyewe, hujitenga na Mungu. Kwa hiyo, kamwe hutamjua Mungu kwa maarifa, huna budi kumjua Yeye kwa imani, kuamini tu; haliji kwa maarifa, ni imani. Mnaona?

199 Kwa hiyo, kila wakati tunapouma hapa . . . Waliuma . . . Kuuma kwa kwanza kulitenganisha ushirika wake na Muumba wake; kisha akauma baruti, inamwua mwe—mwenziwe, rafiki yake; jambo la pili, akauma motokaa, inaua zaidi ya baruti zote; sasa amejiumia mwenyewe bomu la atomiki, sijui atafanya nini na hilo. Unaona?

200 Mungu kamwe haangamizi chochote, mwanadamu, kwa maarifa, hujiangamiza mwenyewe. Kumbukeni hilo, Mungu haangamizi chochote, Mungu ni wa Milele, Yeye haangamizi chochote, bali mwanadamu, kwa maarifa yake, hujiangamiza mwenyewe.

201 Tunapofikia mahali, mnasema, "Vema sasa, hakuna kitu kama Roho Mtakatifu, uponyaji wa Kiungu si wa kweli," kumbukeni tu, unaangamizwa na ujinga wako mwenyewe;

unafikiri ni maarifa, bali ni ujinga. Kwa hiyo u—ulijiangamiza mwenyewe, uliiondoa nafsi yako moja kwa moja kwa Mungu kwa kufanya hivyo. Unaona? Mbona, huyatupi tu chini mawazo yako mwenyewe na kusema, "Ee Hua wa Mungu, njoo uniongoze"? Unaona?

202 Angalia mahali anapokuleta, moja kwa moja kurudi kwenye Neno Lake. "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

203 Sasa, ninataka kujua ni wangapi kwenye mstari huo wa maombi ambao hawanijui, nami—na—nami siwajui, wasionijua mimi, inueni mikono yenu, ninyi ambao. . .? Ni wangapi huko nje wasionijua mimi? Inueni mikono yenu, ama hawanijui, sawa. Huko juu kwenye roshani, na kadhalika, mnaona. Vema.

204 Sasa, kuna ninii tu, kadiri Mungu alivyo Hakimu wangu, watu pekee niwajuao, nimefahamiana na baadhi ya hawa ndugu wa thamani hapa, hasa sana mwenyekiti hapa, Ndugu [Ndugu mmoja anasema, "Hobson."—Mh.] Hobson. Halafu nilikutana na ndugu wengine kadhaa wanaowajua, nami nikawapa wote mikono, lakini, ndugu, nisipopata kuwajua vizuri sana hapa, nitawajua ng'ambo ya kile kidimbwi, tutakapofika Kule, tu—tutaninii. . .Nitakuwa Kule pamoja nanyi, nasi ni wahudumu pamoja.

205 Na baadhi yenu nyote mlikuwa mkihubiri Injili hii nilipokuwa bado maskini mvulana mdogo mwenye dhambi; kwa kweli inahitaji kuwa ni ninyi hapa juu. Lakini ni kitu gani? Mlifyeka vichaka, na—na kuitandaza barabara, kusudi kupiga mbio kuwe rahisi sana kwangu kuliko ilivyokuwa kwenu.

206 Kwa hiyo, ninawatakeni mjue, kwamba ninajua hilo moyoni mwangu. Siku moja tukufu tutakapopeana mikono mezani huko ng'ambo tutaona mahali taji iendapo. Ninyi ndugu mliopiga vita kweli mpate kushinda tuzo, na kunirahisisishia safari, mlihubiri ya kwamba mambo haya yangekuja miaka mingi iliyopita, kabla sijaingia katika huduma, mlihubiri mambo haya yangetukia. Sasa, mnaona, mlitengeneza barabara. Hawa ndio watu mliowahubiria wanaokuja hapa na kuona hasa. Daima mheshimuni mchungaji wenu, yeye anastahili kila heshima unayoweza kumpa, Biblia inasema hivyo. Naam, bwana. "Wala usimfunge kinywa ndama anayepura mahindi."

207 Sasa, huko nyuma muda mrefu uliopita, walipokuwa huko chini pembeni, na kufukuzwa mjini, na kula mahindi kutoka kwenye njia ya reli, ama chochote walichofanya, walikuwa wakitengeneza njia kwa ajili ya jambo hili, wala kamwe msisahau hilo. Wakati hawa wainjilisti wapya wanapokuja na njia ya huduma, usininii. . .Kumbuka, kama ulikuwa unaenda kufanyiwa upasuaji, ungelitaka. . .usingetaka kushughulikiwa na mwanafunzi mpya ambaye hana ujuzi wowote, ungetaka

mmoja aliye na ujuzi. Vipi kuhusu nafsi yako kufanyiwa upasuaji? Hmm? Hiyo ni kweli, ndugu. Hakika ni kweli.

208 Sasa, hii ni karama, hebu niielezee kwa muda kidogo tu sasa, hii ni karama, nji—njia tu niliyo nayo ya kujitoa tu kwa Hua. Ndipo situmii mawazo yangu mwenyewe, macho yangu mwenyewe, maneno yangu mwenyewe, ninatulia tu mbele Zake. Ni karama tu ya kujua jinsi ya kufanya hilo. Na inapokuja, basi hiyo. . . Ni—ningeweza . . . Nimetulia sasa hivi. Mnaona?

209 Na kila mmoja wenu ni roho, kama sivyo, ungekuwa umekufa, kwa hiyo unapokuwa na kutokuamini, ninahisi hilo likiingia, shaka kidogo, unaihisi, lakini wakati kuna imani, unaihisi hiyo, pia. Mnaona? Vema sasa, imani yenu ndiyo inayosababisha maono haya, sasa, Mungu anajua hilo. Imani yako ndiyo inayofanya jambo hilo, sio mimi. Si—siidhibiti, inaniongoza, ninajituliza tu, halafu lolote Yeye afanyalo, ninalisema, mpaka ninapoanza kuwa dhaifu sana, basi ninaweza kujisikia nikijikakamua, ndipo ninaninii tu . . . Na—najua kama nikiendelea, ni muda kidogo tu, mpaka watakaponinii, Ndugu Roy ama Billy Paul hapa, watakaponichukua.

210 Na kwa hiyo basi, nina mikutano mingine, siku zingine usiku, nami ninajaribu kujiondoa. Ni, ka—karama hiyo si kwa ajili yangu, ni kwa ajili yenu. Siwezi . . . Kama nikitaka kujua jambo fulani, ninasema, “Bwana, ni kitu gani? Ni kitu gani?” Yeye haniambii, isipokuwa iwe anataka. Lakini ninapojipumzisha kwa karama, basi mnaweza kuitumia. Sasa, ni wangapi wanaelewa hilo? Hiyo ni imani yako mwenyewe.

211 Sasa, kama utaangalia tu *huku*, kama yule mwanamke aliyegusa upindo wa vazi Lake, na—na kuamini, na kujua ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu . . . Mnaona? Sasa, njia pekee utakayopata chochote kutoka kwa karama ya Mungu, ni kuiendea kwa uchaji na heshima.

212 Vipi kama Martha angalisema, “Hukuwa hapa! Kwa nini hukuja nilipokuita? Ndugu yangu Lazaro amekufa siku nne. Tunaamini wewe ni mnafiki, tusingekuwa na uhusiano wowote nawe”? Lisingetukia kamwe.

213 Vipi kama yule mwanamke Msirofoinike: Wakati Yeye aliposema . . . akasema, “Bwana, mrehemu binti yangu, amepagawa sana na ibilisi.”

Akasema, “Si vema Kwangu kuchukua chakula cha watoto na kuwapa ninyi mbwa.” Whiu!

Wewe ungesema nini? “Mimi, mbwa? Mtakatifu anayejiviringisha, sina uhusiano wowote nawe, nenda zako.”

Sio yeye, yeye alisema, “Hiyo ni kweli Bwana, bali m—mbwa hula makombo chini ya meza ya bwana.”

Akageuka, kasema, “Kwa sababu ya neno hili . . . ” Mtazamo wake. Mnaona?

214 Martha akasema, “Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa, lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.” Loo!

215 Akasema, “Mimi ndimi Ufufuo na Uzima, yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Na kila aishiye na kuniamini Mimi, hatakufa kamwe. Je, unasadiki haya?”

Akasema, “Naam, Bwana,” alimwita kile alichokuwa, Bwana. “Naam, Bwana, ninaamini ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu yule ajaye ulimwenguni.”

216 Ndugu, jambo fulani halina budi kutukia, hivyo tu. “Mmemzika wapi?” Ilikuwa hivyo. Hilo ndilo lililohitajika kufanya hivyo; hilo ndilo linalohitajika kufanya hivyo kila wakati.

217 Sasa, kama tu utamkaribia Mungu kwa uchaji uo huo, wewe uliye huko nje bila kadi ya maombi. . .Nitawaombea tu hawa kwenye mstari, kuwaonyesha tu ya kwamba—ya kwamba itakuwa. . .Mimi, vema. . .Kumbukeni kuitoa saa hii hapo kabla. Huenda nikawa. . .Nitawaombea tu watu hawa walio kwenye mstari wa maombi, na kisha wewe ndiwe unayepaswa kufanya upambanuzi. Wewe—wewe amini tu kwa moyo wako wote, amini tu kwa moyo wako wote.

218 Ninaweza kukwambia kabla mkutano kamwe haujaanza, kabla ya mstari wa maombi kuanza:

219 Unataka kuondokana na hicho kikohozi cha pumu, mama? Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Kama utaamini wala usiwe na shaka, unaweza kupona hicho.

220 Huku nyuma kabisa kuna mtu ameketi, naye huyo mtu ana ugonjwa wa moyo, amekuwa hospitalini. Kama utaamini, bwana, kwa moyo wako wote, Mungu atakuponya. Bw. Howard, amini.

221 Bwana, una kadi ya maombi? Huna kadi ya maombi? Hatufahamiani, sikujui, sijawahi kukuona maishani mwangu, nasi hatufahamiani kabisa. Lolote Huyo alilosema, hilo ni kweli? Kama ndivyo, inua mikono yako. Vema. Yesu Kristo anakuponya. Sasa nenda nyumbani, umeponywa.

Mnaona ninalomaanisha?

Unajisikiaje? Afadhali sasa, dada? Utaacha maskini kukohoa huko sasa, nenda nyumbani, uwe mzima.

“Kama unaweza kuamini.”

222 Unawazia nini, bwana, huko nyuma na ugonjwa huo wa mguu? Unafikiri kwamba Mungu anakupa afya, na kukuponya? Kijana uliyeketi hapo, ukiniangalia, unaamini Mungu atakuponya? Kama unaamini hilo kwa moyo wako wote, unaweza kuupokea. Amina.

Usiwe na shaka, amini.

223 Kuna mama aliyeketi pale akimwombea mumewe, ana tatizo kwenye misuli yake. Unaamini ya kwamba Mungu atampa afya? Kama unaamini, unaweza kupata kile unachoomba, kama utaamini, usiwe na shaka moyoni mwako mwote. Simama, mama, ili watu waweze kuona wewe ni nani, unayeketi huko nyuma. Vema. Amini tu kwa moyo wako wote.

224 Angalieni kile ilichomfanyia huyo mwanamke, angalieni kile ilichomfanyia huyo mwanamume. Wao ni nini? Wao ni wana-kondoo, waliomruhusu Hua aingie. Hivyo ndivyo ilivyo hasa. Mwaminini Mungu.

225 Njoo, mama. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Ama mtumishi Wake, nilimaanisha kusema. Hilo huwakwaza watu wengine, ndio sababu ya mimi kulisema hivyo, mnaona. Unaamini? Hatufahamiani. Vema. Hatujawahi kukutana hapo kabla, nasi, hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana maishani. Sasa, sikujui, wewe hunijui, na kwa hiyo sisi hapa kwa mara ya kwanza, kukutana. Sijui kabisa una shida gani, sina hata fununu kwa nini umesimama hapa. Ni—ningeweza . . . Huenda ikawa, huenda ikawa wewe ni mgonjwa, huenda umesimama kwa ajili ya mtu mwingine, huenda ikawa una matatizo ya kifedha, huenda ikawa ni matatizo ya kinyumbani, huenda ikawa . . . Sijui ni nini, unajua hilo, kwamba sijui lolote kulihusu. Kama hivyo ndivyo ilivyo, kadiri tujuavyo, inua mkono wako ili watu waweze kuona.

226 Mnaona? Sasa, sisi hapa. Sasa mnaona, ni kustarehe tu. Nitazungumza na huyu mwanamke. Sasa, huyu hapa mwanamke, mimi ni mwanamume, nasi tumekutana tu kwa mara ya kwanza maishani, kama vile Yesu na yule mwanamke kisimani huko Samaria, kile kisima. Sasa, Yeye alizungumza naye kwa muda kidogo tu kusudi aishike roho yake. Mnaona? Kwa sababu sasa, inakuja tu kila mahali, kama pigo la moyo, kila mahali, ni wa—watu tu.

227 Sasa, sikujui, na Mungu anakujua Naye ananijua. Sasa, kama Mungu atanifunulia kitu kama Yesu alivyomwambia yule mwanamke shida yake ilikuwa nini . . . Mnakumbuka kusoma hadithi hiyo? Yohana Mtakatifu 4. Naye akasema shida yake ilikuwa ni nini, na alipofanya hivyo, akasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua, sisi Wasamaria, tunajua, ya kwamba yuaja Masihi, aitwaye Kristo, na wakati atakapokuja, Yeye atatwambia mambo haya." Alijua hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi.

Na kwa hiyo, basi akasema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye."

228 Akakimbia mjini na kuwaambia watu habari zake, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?" Nao watu mjini wakamwamini Yeye kuwa ni Masihi kwa sababu ya ushuhuda wa huyo mwanamke.

229 Sasa, hayo ni Maandiko, sivyo? Sasa, wahudumu, hayo ni Maandiko? Vema. Sasa ninyi ni kusanyiko, wala si lazima mwanamke aje kuwaambia, mko hapa kumwangalia. Sasa, utaamini ya kwamba Masihi, Mwana wa Mungu, katika umbo la Roho Mtakatifu yuko hapa, akifanya kazi kupitia kwetu, kama tu vile Yeye alivyoahidi kufanya katika Biblia? Mngeamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi ni kitu gani kingekuzuia? Sema tu, "Mimi ni mwana-kondoo Wako, Wewe ni Hua, uniongoze kwenye afya, Bwana."

230 Sasa, sisemi ya kwamba atafanya hivyo. Lakini, ona sasa, hapa sina budi kuliendea hilo kwa imani, inanibidi kulikaribia nipate kuliamini kwa imani, sasa, huenda Yeye asifanye hivyo. Kwa sababu kwa muda kidogo, nilitaka kuzungumza na kidogo nijirudishe tena kutoka kwenye maono yaliyotukia kwenye kusanyiko. Ili kwamba watu waone haikuwa mstari wa maombi, wala chochote hakikuwa na uhusiano wowote. . . ni wewe huko nje. Ninii tu, Mungu yuko kila mahali. Hivi hamwamini hilo? Yeye yuko kila mahali.

231 Mama huyo anaugua yabisi kavu. Ninamwona akijaribu kutoka kitandani, ni mbaya zaidi asubuhi kuliko wakati wowote, unapojaribu kuamka. Sasa, hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli inua mkono wako.

232 Sasa, yeye haonekani hivyo, sivyo? Lakini anayo. Ni kitu gani? Hilo—hilo ni ono. Nilimwona akifanya jambo fulani, akijaribu, ninaamini, alikuwa akitoka kitandani ama kitu fulani ambacho. . . Sasa, hiyo ni kweli.

233 Sasa, iweni tu na kicho kabisa kwa muda kidogo tu. Huyu mwanamke anahuzunishwa na sababu fulani. Nilikuwa nikitaka kumpita, lakini kuna kitu kilicho ndani sana zaidi ya hilo, ni kwamba ana huzuni, kumbukeni tu. . . kwa sababu huyo mwanamke amezungukwa na huzuni na giza. Loo, naam, ni mpendwa fulani, ni mume wako. Naye yuko hospitalini, Hospitali ya Wanajeshi Wastaafu, katika mji unaoitwa Walla Walla, Walley Walley, ama kitu kama hicho. Hiyo ni kweli. Una kansa. Unatoka Oregon. Jina lako ni Bibi Leverson. Hiyo ni kweli. Unaamini sasa, kwa moyo wako wote? Basi nenda kama ulivyoamini, na iwe kwako, katika Jina la Bwana Yesu.

234 Vema, unaamini kwa moyo wako wote? Amini tu. Usiwe na shaka. Sema, "Bwana, naamini, kwa yote yaliyo ndani yangu ninaamini." Ni wangapi wanaoamini sasa kwa mioyo yenu yote?" Sasa, ni kitu gani kinachofanya hivyo? Yule Hua, yule Hua. Sasa, iweni na kicho. Amininі tu. (Huyu ndiye mgonjwa anayefuata?)

Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini ya kwamba Mungu. . .? Hata nisingalikwambia jambo lolote, unaamini ya kwamba Mungu angekuponya? Njoo hapa.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia mwanamke huyu aponywe kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

Sasa amini kwa moyo wako wote. Kuwa na imani.

Unaamini kwa moyo wako wote? Hata nisingalikwambia jambo lolote, ungali ungeamini kwa moyo wako wote?

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia mtu huyu aponywe. Amina.

235 Njoo ukiamini. Sasa, unajua ya kwamba ninajua shida yako, lakini hata nisingalisema chochote, ungeamini kwa moyo wako wote? Hebu nikuonyeshe tu jambo fulani. Njoo hapa kwa dakika moja. Weka mkono wako juu ya wangu. *Namna hii*, pitanisha tu mkono wako. Una tatizo la kina mama, tatizo la kike. Unaona, kamwe sikupata hilo kutokana na ono, nililipata kutoka *hapa*.

236 Hebu nikuonyeshe kitu fulani. Sasa angalia mkono wangu sasa. Ni kama tu mkono wa mtu wa kawaida, sivyo? Hapa, sasa chukua mkono *huu*, weka mkono *huu* hapa juu yake. Bado ni vile vile. Sasa badilisha leso yako, weka hapa. Sasa sivyo. Unageuka mwekundu, umevimba, vitu vidogo vyeupe vinapitapita juu yake. Sasa nausogeza tu mkono wako, nitaupitanisha tu mkono wangu kwa njia ile ile. Si hivyo sasa. Sasa wewe weka tu mkono *huo* moja kwa moja hapo nyuma tena, namna *hiyo*. Hiyo hapo tena.

237 Sasa, unajua jambo fulani linaendelea pale. Halafu sehemu ya kushangaza, inakwambia shida yako. Sasa, kwa ono ningeweza, kama Bwana angependa sasa hivi, ningeweza kuita ono, na, ungeweza, kumwomba Mungu, lingeendelea tu zaidi na zaidi. Sasa, angalia hili kwa dakika moja tu. Unaamini kwa moyo wako wote sasa, ya kwamba utaponywa?

Bwana, mrehemu mwanamke huyu.

238 Ninamwamuru adui huyu, kwa Jina la Yesu Kristo, ninamtoa, toka ndani yake!

239 Sasa angalia huo mkono sasa. Jambo fulani lilitukia, sivyo? Sasa angalia, wekelea mkono *huu* sasa, jinsi tu ulivyofanya. Sasa ninawekelea mkono wangu. Haubadiliki hata kidogo. Sasa hebu nichukue mkono *huu* tena. Jambo fulani lilitukia, sivyo? Uliponywa. Hivyo ndivyo ilivyo, mnaona.

240 Hivyo tu, hivyo ndivyo tu ilivyo. Yeye si ni wa ajabu? Amini kwa moyo wako wote.

Sasa, nisiposema neno, nikuwekee mikono, utaamini?

Katika Jina la Yesu Kristo, mtu huyu na aponywe.

Njoo, bwana.

Katika Jina la Yesu Kristo, mtu huyu na aponywe.

241 Njoo, dada. Amini kwa moyo wako wote. Una huzuni? Unaamini utaponywa? Unaamini? Vema. Nawe unaamini ya kwamba . . . Je, wewe ni Mhispania? [Huyo dada anasema, “Mimi ni nusu Mjapani na nusu Mhispania.”—Mh.] Loo, ati Mjapani na nani? [“Mhispania.”] Mhispania na Mjapani. Uh-huh. Vema. Je, ulizaliwa hapa? [“Huko Mexico.”] Loo, ninapenda huko chini,

kuzuri sana. U—unampenda Bwana? Unafikiri hicho kisukari kimekwisha, nawe unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima sasa? Vema. Basi endelea, na uwe mzima. Kuwa tu na imani. Mungu akubariki.

242 Nisingalisema lolote, ungeamini uliponywa, kwa vyovyote vile, sivyo? Ungeamini? Lakini unataka u—ugonjwa huo wa mgongo ukuache, na, ili upate afya.

Katika Jina la Bwana Yesu, jalia, Bwana, kwamba aponywe.

Nenda sasa, na uamini mafigo yako yatakuwa sawa, nawe utapona.

243 Vema, sababu ya kuwa na nguvu sana pale, mgongo wako, pia, umekuwa ukikusumbua, kwa hiyo. . .Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, unaamini kwa moyo wako wote sasa? Kama ungeamini kwa moyo wako wote, unaweza kwenda na kuponywa katika Jina la Yesu.

244 Vema. Njoo. Sasa, unajua ninajua shida yako. Kwa hiyo, unaamini ningeweza kukwambia? Una matatizo mengi, lakini jambo muhimu unalotaka liombewe ni yabisi kavu yako. Sasa nenda ukapate afya. Sema tu, "Asante, Bwana Yesu."

245 Sasa, unajua ya kwamba ni—ninajua shida yako. Lakini kama nikikwambia jambo lako muhimu unalotaka niombee, ingekusaidia? Ugonjwa wako wa moyo. Nenda tu uamini, nawe utaponywa. Kuwa tu na imani, usiwe na shaka hata kidogo.

Unaona ninalomaanisha, rafiki? Ni ono, lakini, loo, hilo karibu linakuua. Unaona? Unaamini Yeye yupo hapa? Hakika, Yupo hapa. Sasa na tuombe.

Njoo, dada.

Katika Jina la Yesu, jalia aponywe. Amina.

Nenda ukiamini kwa moyo wako wote.

246 Sasa, bwana, lazima uwe na imani, unajua hilo, kwamba kansa hiyo ingekuua. Lakini unaamini ya kwamba Mungu atakuponya hiyo kansa, nawe utakuwa mzima?

Ninaiamuru hiyo kansa, katika Jina la Yesu Kristo, imtoke! Amina.

Nenda ukiamini sasa.

247 Na kama utakuwa na imani na kuamini kwa moyo wako wote, hutakufa kwa ugonjwa wa moyo, utapona. Unaamini? Vema. Nenda ukiamini, useme, "Bwana asifiwe."

Vema. Unaamini kwa moyo wako wote?

Katika Jina la Bwana Yesu, jalia aponywe. Amina.

Amini sasa.

Kwa ajili ya mtoto? Kama nikimwekea mikono, je, atapona?

Katika Jina la Yesu Kristo, huyu mtoto mchanga na aponywe. Amina.

Usitie shaka, itakuwa sawa, amini.

Rehema! Ndugu, huna budi kuamini, la sivyo ita—itaendelea kula moja kwa moja ndani. Lakini unaamini itakuwa sawa?

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia, ibilisi amwache huyo mtu. Amina.

Kuwa na imani, amini.

Unaamini kwa ajili yake sasa, bwana? Njoo hapa, mvulana mdogo.

248 Bwana, mponye huyu mvulana mdogo. Tujalie, ninapomchukua mikononi mwangu, na kumwekea mikono katika ukumbusho wa yale Yesu aliyowafanyia watoto wadogo. Jalia aponywe, katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa, nenda na usiwe na shaka, naye atakuwa mzima.

Vema. Njoo, bwana.

Baba Mungu, ninaomba ya kwamba utamponya mtu huyu. Jalia hali hii imwache, katika Jina la Yesu. Amina.

Amini. Sasa amini tu kwa yote yaliyo ndani yako.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu na aponywe. Amina.

Vema. Njoo, bwana. Utaamini?

Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yangu na aponywe. Amina.

Amini sasa, usiwe na shaka, amini kwa moyo wako wote.

Vema, njoo, mama.

249 Unanyamazia nini? Je, unajua Mungu anambariki tu kila mtu? Kama sikuliwazia, ningewakomesha. Mnaona? Inaendelea vivyo hivyo. Ni ninii tu, wewe—wewe . . . Mnaona, jambo lenyewe ni kwamba, mnaona, pale . . . Ni wangapi wanaojua hapana budi kuwe na Kitu fulani mbali na Ndugu Branham kinachofanya hivyo? Inua mkono wako. Unajua nisingeweza kufanya hivyo. Vema, basi kuna namna fulani ya upako hapa. Hiyo ni kweli? Mnaamini ni yale Biblia iliyosema? Mnaamini hilo? Vema basi, je, Yesu yeye yule aliyetoa ahadi hiyo, Hua yule yule, hivi Yeye hakusema, "Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya"?

250 Hilo ono karibu tu, karibu linaniua. Mnaona? Ni wangapi wanafahamu Biblia inafundisha hivyo? Mbona, hakika, mtu yeyote anayeijua Biblia anajua hilo. Ni ninii tu, siwezi kusimama kwa kila mmoja. Lakini ukifanya hivyo, lazima ujue ya kwamba Mungu ni yeye yule tu, Ro—Ro—Roho Mtakatifu aliponena nami huko juu (Kama mtanipa tu muda kidogo wa kujirudisha nyuma kidogo.), Yeye alisema, "Ulizaliwa kuwaombea wagonjwa, kuzaliwa kwako kwa njia ya kipekee."

251 Nuru hiyo, mnayoiona kwenye ile picha ilikuwa ikining'inia kwenye kitanda changu nilipozaliwa. Nilizaliwa kwenye godoro dogo la nyasi kavu na mto wa makapi. Mama yangu alikuwa na umri wa miaka kumi na mitano, baba yangu alikuwa na kumi na minane. Saa kumi na moja asubuhi, hawakuwa na dirisha ndani ya nyumba, walikuwa na kijilango kidogo. Sijui kama mumewahi kuona. . . Ni wangapi wenu wamewahi kuona mojawapo ya hivyo, kama, vinavyochukuliwa kuwa kama dirisha, bali ni kijilango kidogo tu unachofungua.

252 Na—na Malaika huyo wa Mungu, kwenye saa kumi na moja asubuhi, tarehe 6 Aprili, 1909, saa kumi na moja asubuhi, aliingia moja kwa moja na kusimama juu ya kile kitanda kidogo nilimokuwa nimelala. Hawakujua ni kitu gani. . . Watu wangu walionitangulia walikuwa Wakatoliki, na kwa hiyo, hapakuwapo na makanisa ya Katoliki huko juu, na kwa hiyo wakanipeleka kwenye kanisa dogo la Kibaptisti, na huko nikahudhuria kanisa kwa mara yangu ya kwanza. Hilo kanisa la Kibaptisti linaitwa Kanisa la Kibaptisti la Ufalme wa Oposamu, Kanisa la Kibaptisti la Ufalme wa Oposamu. Na huko ndiko nilikohudhuria kanisa kwa mara yangu ya kwanza. Na tangu nilipokuwa tu na umri wa yapata miaka miwili, ono la kwanza lilikuja, tangu hapo limekuja, na kuendelea, na kuendelea, na kuendelea, nami nina umri wa miaka hamsini na mmoja sasa. Kwa hiyo, mnaona, ni—ni yale maono.

Wakati aliponiambia, Yeye alisema, "Ulizaliwa kwa kusudi hili, kuwaombea wagonjwa."

Nikasema, "Hawataniamini."

253 Akasema, "Kama Musa alivyopewa ishara mbili, wewe umepewa ishara mbili." Akasema, "Mojawapo, washike tu watu mkono wala usitumie mawazo yako," mnaona, kasema, "nawe utaambiwa shida yake."

254 Vema, nilifanya hivyo, niliangalia jinsi mambo yalivyoenda kwa muda, nikiwaangalia watu. Halafu basi, nikawaambia ya kwamba hili lingine litatukia, sasa mnaona linatendeka. Sasa, kitu kingine kinaingia, mnaona, labda zaidi sana yote yatakuwa huko ng'ambo, maana ninaihisi ikivuta ng'ambo.

255 Lakini sasa, ili mpate kujua ya kwamba ni Mungu, ni Yeye. . . Ni ninii. . . Ndugu, dada, ono hilo, Malaika huyo, Mungu Mbinguni anajua hilo ni kweli. Ingenifaa nini kusimama hapa nje, kuwaambia ninyi watu mambo haya? Si—silipwi kwa hilo, mnajua hilo, kanisa langu hunilipa. Sadaka zangu za upendo ni misheni za ng'ambo, mimi, mwulizeni katibu hapa, mimi, hiyo ni kweli, mnaona, siioni kamwe, inaenda ng'ambo, ninaenda kule kuhubiri Injili, katika nchi zingine.

256 Gharama hulipiwa, hao ndugu, mwenyekiti na hao wengine wanaweza kuwaambia, sipati pesa. Si—sinazo. Ninapata dola mia moja kwa juma kutoka kanisani mwangu. Vema, ninapata

hizo nikikaa tu nyumbani, nikienda kuvua samaki kila siku, na kuchunga kanisa Jumatano usiku na Jumapili asubuhi, mnaona, kwenye maskini maskani ya Baptisti. Hiyo . . . Si pesa.

257 Kama ikiendelea, iwe ni pesa, ningeweza kuwa milionea, kama ningalitaka kuwa. Ni—nilipewa dola milioni moja, laki tano katika toleo moja, wakati mmoja, si wote . . . kutoka kwa mtu mmoja. Hiyo ni kweli. Mawakala wa FBI waliniletea. Nilitoa hicho kipande kutoka gazetini na kadhalika. Nikasema, "Hata ninakataa kuiangalia." Nikasema, "Sitaichukua. La, bwana. Siitaki."

258 Kwa hiyo ninasimama hapa kwa sababu gani? Ni kwa nini siko nyumbani na familia yangu na kadhalika, ningekuwa afadhali zaidi, na kuishi maisha kama hayo badala ya kuiacha familia, na kufanya kazi, na kuchoka, na kulia, na kuvuta, na kushawishi? Ni kwa sababu kwamba nina agizo, sina budi kulitekeleza.

259 Mara nyingi, wenye kushuku, watu wanaoinuka, na—na—na watu wakisema, "Loo, ni bure," hilo—hilo ni ninii sana . . . hilo linaumiza, mnaona.

260 Lakini ni mamoja tu, kwamba, siombi nipate njia rahisi, ninalitarajia. Naam, bwana. "Lazima nipige vita, ikinibidi kutawala." Naam, bwana. Sina budi kufanya hivyo, Bwana wetu alifanya. Kwa hiyo niko hapa kujaribu kuwasaidia. Na vizuri sana nijuavyo, ninajaribu kuwasaidia.

261 Na tafadhalini mniamini, kama nikisema lolote, halafu Mungu analiunga mkono na kusema ni kweli, Biblia ilisema "msikieni, kwa kuwa niko pamoja naye." Hiyo ni kweli? Sasa, ninawaambia ya kwamba kila mmoja wenu anaweza kuponywa, tayari mumeponywa, kama tu ukitambua jambo hilo. Hiyo ni kweli.

262 Sasa, ni nani anayefuata? Mwanamke huyu hapa? Hapa. Kama vile, mama huyu hapa . . . Sasa angalia, mama, hatufahamiani. Sikujui, lakini unajua ya kwamba ninajua shida yako. Nisingalisema lolote juu yake, bado, unaamini ungeponywa, kwa vyovyote vile? Unaamini? Hiyo—hiyo ndiyo njia ya kuliamini, hiyo ndiyo njia.

263 Una matatizo, una matatizo kadhaa. Hiyo ni kweli. Viungo vyako vinakakamaa, umekuwa hivyo kwa muda mrefu sana. Ninaona mgongano, au, loo, ni ajali ya motokaa iliyosababisha hilo. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Je, hiyo ni kweli? Inua mkono wako, kama hiyo ni kweli? Unaona? Ni, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Hivi huamini hilo?

Katika Jina la Yesu, nenda ukaponywe, dada. Amina.

Njoo, ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu, nenda ukaponywe. Amina.

Njoo, dada yangu.

Katika Jina la Yesu, jalia roho aliye juu yangu amtie mafuta huyu mwanamke, Bwana. Mungu, katika Jina la Yesu, jalia waponywe. Amina.

Njoo, ndugu.

Katika Jina la Yesu, na aponywe. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

264 . . . utaamini, ndipo ugonjwa wako wa mgongo utaondoka, pumu yako itaondoka. Unaamini hilo? Una tabia unayotaka kuacha, kuvuta sigara. Umeziacha? Kwa moyo wako wote? Kama nikikwambia wewe ni nani, utafikiri kweli imekwisha basi, sivyo? Bw. Cunningham. Nenda zako ukashangilie, useme, “Asante, Bwana.” Uponywe.

Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa, wekeaneni mikono, ninyi nyote hapa ndani.

Ee Hua, njoo Hua, uwashukie wana-kondoo Wako, Bwana.

Loo, enyi wana-kondoo, ongozweni na Hua, mpate afya.

265 Shetani, umeshindwa, watu watatambua baada ya kitambo kidogo, ya kwamba umeshindwa, huna uwezo juu yao. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yuko hapa, Naye alikushinda, umeshindwa, umeshindwa kwa miaka elfu mbili. Toka ndani yao katika Jina la Yesu Kristo!

60-0805 Mwana-kondoo Na Hua
Eisenhower High School
Yakima, Washington Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org